
VBS
MATUKIO YA NGAMIA
Kuwa jasiri pamoja na Danieli na Marafiki
MWONGOZO WA MKURUGENZI

# MATUKIO YA NGAMIA

Kuwa jasiri pamoja na Danieli na Marafiki

Shule ya Biblia ya Wakati wa Likizo (VBS)

Kutoka kwa

Watoto ni Muhimu

## MWONGOZO WA MKURUGENZI

Tovuti: childrenareimportant.com/camels

## SHUKRANI KWA TIMU YOTE YA "WATOTO NI MUHIMU"!


Founders, Dwight y Kristina Krauss
Creative Team Manager, Flor Boldo
Creative Editorial Team, Jennifer Sánchez, Areli Salinas, Ramón Martínez, Marlon Hernández.
Designer, Julio Sánchez
Contributing Designer Suzanna Kangas (Suki)
Consulting Emeritus, Miguel y Vickie Kangas
Facebook Page Spanish Admin, Ramón Martínez and Verónica Toj
Facebook Page English Admin, Marlon Hernández and Flor Boldo
Translation Team, alineviera, Annupama Wankhede, Anton Klymyk, Araz Mammadzadeh, Aroma Publications and Media, Arturo Jr Boron, Blessy Jacob, Carmela Dawn Flores, Chrisbresnahan, David Raju, Ephraim Njuguna Mirobi, Finny Jacob, Geenav, HamidReza Azimi (hamid.azimi1364 at gm#ail com), Heyaudrey, I-clever.com, iqbalman, Jacob Kuruvilla, kamilturk, Karunguru Mwangi, kiran, Maitrayi Mondal, Marco Chu, Marcos Rocha, Mathew Das, Mitesh Mandaliya, mrramlama, Mrs.Geethashree NavaneethaKrishnan, Nassim Bougtaia, nicbenk, Paul Mwangi, Paul Septan, Rana922, Rubina Rai, Safdar Khan, shahroshan15, Talento-Unido, ueritom, Verdia Juliansyah Cancerika, Yeoh Jung Chin, Zeina Mirella Barzaga Arencibia

# KARIBU KWA MATUKIO YA NGAMIA!

Karibu kwa “Matukio ya Ngamia,” programu mpya ya VBS inayosisimua! Wapeleke watoto wako kwa matukio ya porini yayosisimua yaliyo na ngamia na milki huku tukisoma jinsi ya kuwa kumfuata Mungu kwa ujasiri katika ulimwengu uliojaa maovu, kama vile Wanaisraeli walivyofanya wakiwa kwenye utumwa. Katika programu hii, tutafuata maisha ya Danieli na marafiki zake Shadraki, Meshaki na Abednego. Malkia Esta pia anakuja kama mgeni katika somo lenu la 4 la VBS.

Katika kila siku ya VBS hii, watoto watapenda sana kujua ngamia wanaofurahisha (vikaragosi au waigizaji) na katika namna za kisasa zilizopinduliwa katika maisha. Furahia nyimbo halisi za sinema ambazo zinaimarisha mada ya VBS hii. Wafunze watoto utendaji unaosisimua unaoambatana na mada ya somo na uurudie katika somo lote kuu na katika siku yote. Unda vifaa vya ufundi vinavyosisimua kwenye Vifaa vya kituo katika Milki, tumia nyenzo za bei nafuu ambazo ni rahisi kupata au ni rahisi kutumika kwa namna mbadala katika eneo lolote katika ulimwengu. Darasani katika Kasri, watoto wataburudika kutatua mizingile migumu na mafumbo tofauti. Watoto wakubwa watapata nafasi ya kuwaza kuhusu masuala halisi katika maisha yanayohusiana na somo, na kila mtu atapata kazi ndogo ya ziada ya kufanyia nyumbani ili kumsaidia kufanya mazoezi ya somo. Watoto watafurahia kukutana na Danieli na Esta na kusikia simulizi za Biblia moja kwa moja kutoka kwao, halafu kufanya shughuli inayosisimua katika kituo cha Danieli. Hakika, hakuna VBS inayoweza kuwa kamilifu bila michezo! Pata michezo na wazo tofauti za vitafunio katika Michezo ya Bustani na Vituo vya Karamu za Kifalme. Usisahau kuangalia mawazo ya ziada ili kurembesha VBS yako na kuifanya ya kusisimua hata zaidi!

Kanisa lako linapoendelea na masomo haya matano, tafuteni uhusiano baina ya upendo na ujasiri na kutambulisha sifa hizi kwa wanafunzi.

1 Yohana 4:18 “Katika upendo hakuna woga; upendo uliokamilika hufukuza woga wote, kwa sababu woga hutokana na adhabu. Mtu mwenye woga hajakamilishwa katika upendo.”

Tunapokua kama Wakristo katika kuelewa nguvu za Mungu na upendo Wake mkubwa kwetu, tutaimarika katika ujasiri wetu wa kumtii. Upendo wa Mungu na kwa watu wengine utakua ndani yetu sote, upendo ambao unatuelekeza kwa mambo ya ujasiri kama jinsi walivyofanya Danieli na marafiki zake, na kama jinsi Yesu alivyotufia msalabani.

Somo muhimu zaidi katika programu hii ni somo la 2 lililo na ujumbe wa uokovu. Waalike watoto zaidi katika VBS yako na uwape fursa ya kukabidhi Yesu maisha yao. Hata kama itakuwa ndilo jambo pekee mtakachofanya, VBS yako itakuwa na ufanisi mkubwa. Tafakari ukikutana na watu mbinguni kisa VBS yako! Na tafakari jinsi ambavyo Mungu atafurahishwa nawe kwa sababu uliwaalika watoto hawa ambao anawapenda sana!




Tunamwomba Mungu kuibariki VBS yako sana unapofuata amri ya Bwana ya kwenda na kupata wafuasi wa mataifa yote na kuwafunza watoto kumtii. Lengo letu katika idara ya watoto sio kuwatunza watoto bure wakati wa likizo, ila ni kuchukua kila nafasi kuwafunza watoto kuhusu Mungu. Leta pamoja timu yako ili kuombea shughuli za VBS, halafu tazama jinsi Mungu atakavyotenda katika maisha ya wanafunzi wenu.


Uko hapa kubadilisha maisha; tuko hapa kuwasaidia.

Kutoka kwa timu nzima katika Idara ya Watoto ni Muhimu.

# Muhtasari

## 1. UJASIRI UNAMWEKA MUNGU MBELE






### Danieli 1: Makaazi na shule mpya

Warumi 12:2 “Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu.”

## 2. UJASIRI UNAMWAMINI MUNGU





### Danieli 3: Jaribu la Moto

Zaburi 47:2 “Kwa kuwa BWANA Aliye juu, mwenye kuogofya, Ndiye mfalme mkuu juu ya dunia yote.”

## 3. UJASIRI UNASEMA UKWELI





### Danieli 4: Ndoto iliyo na habari mbaya

1 Wakorintho 13:6 “haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli.”

## 4. UJASIRI UNAWAWEKA WENGINE MBELE YA UBINAFSI





### Esta 3-9: Uokovu kwa watu wake

1 Yohana 3:16 “Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu.”

## 5. UJASIRI UNASTAHIMILI





### Danieli 6: Kujitolea kuomba kila siku na pango la simba

Waebrania 10:36 “Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi.”

# Jinsi ya kutumia nyenzo hii

## MWELEKEZI

Kama mwelekezi wa VBS, jukumu lako kuu ni kuendesha VBS. Kwa kutumia ratiba, programu, na kuratibu waliojitolea na nyenzo, hutakuwa na wakati wa kuendesha shughuli yoyote katika VBS. Sajili watu wa kujitolea na kuwapa washirika wa kanisa majukumu ya sehemu tofauti za VBS. Hatua hii itaongeza msisimuko kuhusu programu na kusaidia washirika kanisa lako kushiriki katika kuwafikia watoto hawa.

## USAJILI

Sajili watu wengi uwezavyo kutoka kwa kanisa lako. Usiombe usaidizi wa jumla katika VBS ila zungumza na kila mtu binafsi na kumwomba usaidizi katika jambo mahususi. Huenda kuna mtu katika kanisa lako ambaye aatahisi woga kufunza lakini atafurahia kuwasaidia watoto kwa ubunifu.

Hapa kuna majukumu yanayopendekezwa (Watu zaidi ya 10):

- MC, "Msimamizi wa maonyesho" – anaweza kuwa mwelekezi wa VBS
- Waigizaji/wachezeshaji vikaragosi 2 katika sarakasi ya ngamia, na mtangazaji (mtu yeyote)
- Kiongozi wa muziki ili kufunza watoto nyimbo za utendaji
- Mwalimu wa somo kuu na watoto wote pamoja– anaweza kuwa mwelekezi wa VBS
- Mwalimu wa kituo cha darasani wa vitabu vya wanafunzi na majadiliano na wanafunzi wakubwa
- Waigizaji 2 kwa Danieli na Esta katika sarakasi na kituo cha Danieli
- Kiongozi wa shughuli katika Sarakasi na kituo cha Danieli
- Kiongozi wa usanifu
- Mratibu wa vitafunio
- Kiongozi wa michezo

Ukiwa na watu zaidi, unaweza kuwa na zaidi ya msaidizi mmoja wa kushirikiana na watoto, kuendesha vifaa vya sauti na picha, kufunza muziki au wasaidizi katika kila kituo, na kadhalika.

## MAFUNZO

Waliojitolea watafurahia zaidi kushughulikia sehemu zao iwapo wataelewa kwa kina kile wanachokifanya. Ratibu siku ya mafunzo kwa kutumia video zilizo katika kituo chetu cha YouTube. Wape maelezo ya kina kuhusu VBS kama vile ratiba na vile vile maelezo mahususi ya sehemu yao katika VBS.

https://www.youtube.com/c/Childrenareimportant

## UALIKAJI NA USAJILI

VBS ni fursa kubwa ya kueneza injili.  Hebu fikiria siku moja ukutane na mtu akueleze kwamba anamfuata yesu kutokana na VBS yako! Usidhibiti VBS yako kwa watoto wanaohudhuria kanisa. Unda nyenzo za matangazo na uwaombe watoto waalike watoto wenzao kuja katika VBS. Iwapo unatoza malipo madogo ya kuingia katika VBS yako, waalike wazazi kutoa ufadhili wa kifedha kwa marafiki wa watoto hawa ili waweze kumjua Yesu pia.

Fanya usajili mdogo kabla ya wakati huu kufika ili kukadiria ni watoto wangapi watakuja kwa VBS yako ili uweze kukusanya nyenzo zinazohitajika.

## RATIBA

Ratiba inafanana katika siku zote 5. Jihisi huru kurekebisha ratiba hii kama inavyohitajika.

Fungua siku pamoja na watoto wote.

Fungua (Wote pamoja):

- Maombi
- Wimbo (kwa hiari)
- Tambulisha kupiga makofi/jambo la kumakinisha
- Sarakasi ya Ngamia
- Nyimbo
- Somo

Tunapendekeza mwimbe nyimbo kadhaa kati ya sarakasi ya ngamia na somo kuu ili kuwapa watoto fursa ya kutembea na kuzunguka mahali walipo.

Kisha wagawanye watoto katika vikundi vya vituo vya mzunguko.

Mzunguko (Vikundi vya Rika)

- Darasa katika Kasri (Vitabu vya wanafunzi)
- Sarakasi na Danieli
    - Sarakasi – Danieli, Esta
    - Shughuli
- Usanifu katika Milki

Kisha watoto wote wanaweza kushiriki katika shughuli za kufunga.

Kwa pamoja, kikundi kikubwa:

- Vitafunio
- Nyimbo (kwa hiari)
- Michezo

Funga siku kwa kupitia kwa haraka funzo na maombi.




## SARAKASI ZA NGAMIA

VBS hii iko na sarakasi 2 kila siku! Ya kwanza ni onyesho la kikaragosi lililo na ngamia wawili, watoto wote wakiwa pamoja, siku inapoanza. Ya pili ni mahojiano na mwigizaji anayecheza jukumu la Danieli katika kituo, baadaye katika siku. Soma zaidi kuhusu michezo ya Danieli katika maelezo kuhusu vituo vya mzunguko.



Watoto wako watapenda kujua marafiki wetu wawili wa ngamia katika maonyesho ya vikaragosi kila siku! Sarakasi hizi halisi zimeundwa ili

kuonyesha sababu ya kila somo. Utahitaji vikaragosi viwili vya ngamia (au waigizaji) na sauti ya mtangazaji huko nyuma ya maonyesho.

- Kameloti: Ngamia mvulana mpumbavu anayependa kutisha, ananuka, na ana njaa wakati waote.
- Kamelia: Ngamia msichana ambaye kidogo hajipendi ila anampenda Mungu, vitu za wasichana, na kucheza densi.
- Mtangazaji

Jihisi huru kubadilisha majina ya wahusika, kuongeza vichekesho, au kurekebisha sarakasi kulingana na mahitaji yako. Tafadhali kumbuka kuwa watoto huwa wanamakinika kwa takariban dakika 8, kulingana na umri wao (dakika 1 kwa kila mwaka wa umri). Maliza sarakasi katika muda wa kipindi hicho, na watatazamia sarakasi wiki mzima. Na usisahau kuburudika!

Unda vikaragosi vyako vya ngamia kwa kutumia violezo rahisi ambavyo unaweza kupakua kutoka kwa tovuti hii ya VBS. Pia tafuta hapa video fupi ya maagizo kuhusu jinsi ya kuchezesha kikaragosi: https://youtu.be/G7NWA7VUZAI

## NAMNA ZA KUMAKINISHA

Kila siku tumetoa tendo la kumakinisha watazamaji. Kila wakati unaposema mada ya somo, kwa mfano, “Ujasiri unamweka Mungu mbele!” wanafunzi wanarudia maneno haya huku wakifanya matendo. Wafunze namna hii ya kuwamakinisha siku inapoanza, yarudie mara mingi katika siku, na kufanya marudio ya matendo ya siku iliyopita. Tazama video zetu za YouTube kwa maonyesho wazi ya matendo.

# VITUO VYA MZUNGUKO

“Vituo vya Mzunguko” ni namna ya kupanga VBS yako ili usihitaji gundi, penseli, n.k kwa wingi kwa watoto wote kuunda usanifu kwa wakati mmoja. Wagawanye watoto katika vikundi 3 au zaidi na uwaambie wabadilishane shughuli. Kwa mfano, unaweza kuambia madarasa Gumu Zaidi na Gumu kuunda usanifu huku darasa la Wastani likisoma kitabu cha wanafunzi na darasa Rahisi likifanya shughuli katika kituo cha “Sarakasi na Danieli.” Kila kituo kimeundwa kuwa cha angalau dakika 20. Mwelekezi au mtu aliyepatiwa jukumu la kusimamia vituo atakuwa akifuatilia saa na kutangaza wakati wa kubadilishana shughuli.

Iwapo kutakua na nafasi ya kutosha, dumisha shughuli moja katika sehemu moja na uwaambie watoto wabadilishane kila baada ya dakika 20.  Hatua hii inawapa watoto wakati wa kusimama na kutembea. Iwapo hakuna nafasi ya kutosha, basi waruhusu wanafunzi wakae sehemu moja ila ubadilishe shughuli wanazozifanya. Wakubalishe kusimama na kujinyoosha au kubadilishana viti baina ya shughuli ili kuwapa fursa ya kutembea.

Mfano:

**Dakika 20 za kwanza**




**Dakika 20 za pili**




Iwapo uko na nafasi ya kutosha, jumuisha Michezo kama kituo kingine ya kubadilishana ili kugawanya marika yote 4. Ratibu muda wa vitafunio katikati ya vituo vya mabadilishano.

Baada ya kuamua ratiba na eneo la kufanyia shughuli tofauti, weka ratiba ile ile kila siku. Watoto watajifunza kwa haraka sana na watajua jambo linalofuata, hata kabla ya kuambiwa na walimu. 😉

Tumia eneo lililo na meza au viti kama vile Darasa katika Kituo cha kasri.

## DARASA KATIKA KASRI

**Mafumbo**




Katika kituo hiki, wanafunzi wataburudika wakitatua mafumbo katika vitabu vya wanafunzi. Vitabu vyetu vimeundiwa kwa umri huu:

Rahisi – miaka 4-6
Wastani – miaka 7-9
Ngumu – miaka 10-12
Ngumu Zaidi – miaka 13+

**Kazi ya ziada**

Katika VBS ya Matukio ya Ngamia, kila somo linajumuisha kazi ndogo ya ziada ya kufanyia mazoezi somo la siku hiyo. Waulize watoto iwapo walikamilisha kazi ya ziada ya jana, halafu mjadiliane namna mahususi za kukamilisha kazi ya ziada ya leo.

Yakobo 1:22 "Basi muwe watendaji wa neno na wala msiwe wasikilizaji tu, ambao wanajidanganya wenyewe."


**Maswali ya Majadiliano**

Watoto wanapoendelea kukua, wanaanza kutambua ugumu wa maisha na wanaweza kuhisi ugumu kutumia hadithi za Biblia katika maisha yao. Kwa sababu hii, tumetoa sehemu ya swali na majibu kwa wanafunzi wakubwa ili kuwaongoza katika baadhi ya maswali haya na kufanya darasa lao kuwa halisi. Usiwape majibu ya mifano mara moja, ila waache wanafunzi wawaze wao wenyewe, hili linawafanya wakumbuke vizuri zaidi walichokisoma. Iwapo inawezekana, usiwape jibu kamwe ila uongoze majadiliano yao ili waweze kupata hitimisho linalofanana wao wenyewe. Wahimize wawaze kuhusu jinsi ya kutumia masomo hayo katika maisha halisi ya sasa ila sio katika mambo ya kihistoria katika Biblia pekee. Unda mazingira ya kuaminiana katika darasa ili wanafunzi wako wajihisi salama kukueleza wanachofikiria bila woga wa kukosa. Watakomaa zaidi iwapo watayajibu maswali haya kibinafsi na kwa ukweli.

## SARAKASI NA DANIELI



Kituo hiki kina shughuli mbili zitakazochukua muda unaotoshana na vituo vinginevyo. Kwanza ni sarakasi na Danieli, kisha shughuli ya kuwasaidia kuimarisha somo. Watoto watafurahia kukutana na Danieli na Esta kutoka kwa Biblia. Tafuta namna zinazosisimua za kuwavalisha waigizaji watakaojitolea kuigiza majukumu haya.
Danieli ni mtu aliye na cheo kikubwa katika milki za Wababiloni, Wamidiani na Waajemi. Esta ni malkia mrembo wa milki ya Waajemi. Tumewasilisha simulizi kadhaa kwa sarakasi. Jihisi huru kugeuza sarakasi kama inavyohitajika au kuibadilisha kuwa mahojiano na mwalimu. Iwapo kuna watu wa kutosha, pia unaweza kumwalika Shadraki, Meshaki na Abednego au Mfalme Nebukadneza kuwatembelea.



Baada ya sehemu ya sarakasi ya kituo, fanya shughuli hii na watoto. Shughuli hii ni kifaa cha kuburudisha ambacho kitawasaidia kuimarika katika walichokisoma. Kila shughuli inaendana na somo la siku hiyo. Kitu kikubwa kuhusu shughuli hii ni kuwa bali na kusisimua pia ni fursa ya wanafunzi kufikiria na kuwaza kuhusu wanachoweza kufanya katika matukio tofauti.

## UFUNDI KATIKA MILKI

Mtaburudika katika kituo cha Milki, wakati wa kufanya mazoezi ya ubunifu katika sanaa na vifaa rahisi. Kila ufundi umeundwa kwa watoto wote wachanga na wakubwa; kila mtu ataburudika kuuweka pamoja na kutumia ubunifu wao binafsi.




## KARAMU YA KIFALME

Katika kituo hiki unaweza kuwapa vitafunio vya lishe bora, vitamu na vinavyoburudisha katika kila somo. Uko na hiari ya kubadilisha kiungo chochote na kukifanya kuwa kitu kinachoweza kutumika ili kuhakikisha ni kirahisi na cha bei nafuu. Bali na kuwa vitafunio, pia linawasaidia wanafunzi kuunda vitafunio hivi kama shughuli nyingine ya kuimarisha somo hili.



## MICHEZO YA BUSTANI

VBS haiwezi kukamilika bila michezo! Katika kituo hiki, utapata michezo inayosisimua na iliyo na utendaji mwingi. Watoto wataburudika kuicheza na itakuwa rahisi kwenu kucheza. Michezo hii inahitaji nyenzo za bei nafuu zilizo rahisi kupata. Burudika katika mazoezi haya katika VBS hii inayosisimua.



### MAHALI PA TOFALI

Kuta za matofali za kurembesha, kuiga kasri



### MLO KATIKA KASRI

Unaweza kuwawekelea watoto taji, rembesha meza na kitambaa cha meza. Huku watoto wakikula kitafunio kitamu, watajihisi kana kwamba wanakulia kwenye kasri





### NGAMIA WA KADIBODI

Unaweza kuunda ngamia kadhaa wadogo wa kurembesha viti au meza za kazi za watoto



### GURUDUMU LA SHUGHULI

Unda mchezo wa kuzungusha ambapo unaandika virai vya matendo ambavyo watoto wanaweza kujizoesha, uweke mahali popote katika chumba, utakuwa pambo nzuri la kucheza nalo







### TANURI

Unda tanuri kutoka kwa sanduku la kadibodi kwa somo la 2 kama sehemu ya kupamba chumba. Wakati huo huo litaburudisha watoto.

### FREMU YA PICHA

Unda eneo la picha ili watoto wapige picha aina ya selfie.



### PANGO LA SIMBA

Pamba sanduku la kadibodi kwa kuweka karatasi ya kijivu au hudhurungi katika pande ili kuiga kuta za pango. Eneo la nyuma bandika picha kadhaa za simba na mtu anayewakilisha Danieli, na mtakuwa na pango la somo la 5. Itakuwa sehemu ya kupamba darasa lenu na mnaweza kuitumia katika shughuli fulani.



### KITI CHA KIFALME

Pamba kiti kifanane na kiti cha kifalme.





### BUSTANI ZA KARATASI

Bustani zinazoning'inia za Babeli zinaweza kuwa himizo la mapambo na mazingira ya darasa. Watoto watahisi kana kwamba wako Babeli!

### MAPAMBO YA NAMNA YA KUNEI

Unda ufundi wa namna ya kunei na wanafunzi wako na uviweke kote chumbani kama mapambo yaliyo halisi sana.





### MOTO WA KARATASI

Tandaza zulia au blanketi rembo katika sakafu kwa mviringo, weka mito juu yake na kisha moto wa karatasi hapo katikati. Tumia nafasi hii kuwasimulia kuhusu maisha ya viongozi wa VBS hii nzuri. "Matukio ya Ngamia"



# 1 USHUJAA UNAMWEKA MUNGU MBELE

## Danieli 1: Makaazi na Shule mpya

### VIMAKINISHI / MAKOFI 1

"Ushajaa unamweka Mungu mbele"

1. "Ushujaa" = Inua mikono kwa namna ya kunyoosha ngumi
2. "Unamweka Mungu" = Piga makofi mara mbili
3. "Mbele" = Nyoosha kidole hadi kwenye anga

### MSTARI WA KUMBUKUMBU 1

*Warumi 12:2 "Wala msiifuatishe namna ya dunia hii; bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mpate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu."*

### SARAKASI 1: MASHINDANO YA NGAMIA

Kamelia anaingia katika mandhari: Lo, waone ngamia hawa! Ninafurahia kutizama shindano hili kubwa. Ewww, nini hiyo inanuka?
Kamelot katika mandhari: Pole, nilisahau kuweka marashi leo. Naweza kuwa na mnuko mkali. Je, jina lako ni nani bibi?
Kamelia: Ni Kamelia. Na, je wewe bwana?
Kamelot: Kamelot, Yuko tayari kukimbia! Nimekua nikifanya mazoezi mwaka wote: kukimbia na kukimbia na kukimbia (ala!) na kuteleza na kukimbia na labda kunywa maji kiasi wiki ifuatayo na kutafuta picha katika mtandao wa Google na kukimbia na kuota kuhusu kukimbia na kukimbia…
Kamelia: Lo, huku ni kukimbia kwingi! Umeibeba nini mgongoni?
Kamelot: Rafiki yangu roboti nami tuko nambari 7, ona? Ila sielewi ni kwa nini roboti yangu inasema kama mkubwa wangu.
Ewe, Niliskia kwamba baadhi ya ngamia hao wakubwa pale wakizungumza kuhusu dawa kuwa yenye nguvu na kasi. Nikidhani inaitwa … Sredoid? Blefoid? Zephalapoid? (Kamelot anashindwa kutamka neno steroidi.) Kudanganya kidogo hakumdhuru yeyote, kuna mdhuru? Siwezi kushikwa… niko na mbio sana, haha!
Kamelia: Hilo ni ujeuri kwa wengine. Fanya kila uwezalo kumweka Mungu mbele kwa kumtii na kuwatendea wote kwa usawa. Vilevile, iwapo utashinda au la. Mungu atakuwa nawe. Je, si huo ndio ushindi mkubwa unaweza kuwa nao?
Kamelot: (lo) Kweli. Basi, niliweza kukimbia hadi mstari wa kwanza! (Anatoka jukwaani, anateleza na kuanguka) Niko sawa!
Kamelia: Natumai kutaenda vizuri! (Kamelia anamshangilia rafikiye kutoka jukwaani)
Mtangazaji: Na ndio hao wameanza! Nambari 3 anaanza kuongoza, anafuatwa na nambari 1. Na ndio huyo nambari 27! Nambari 3 anang'ang'ana kukaa katika nafasi yake. Ni mita 100 pekee zimesalia… Nambari 27 amempita nambari 1…. Naaaa ni nambari 3 ameshinda! Huku akifuatwa na Nambari 27 na nambari 1!
Kamelot anaingia huku akihema.
Kamelia: Nyinyi wote mlikimbia haraka sana njiani! Ilifurahisha kuwaona. Je, kuliendaje?
Kamelot: Hata sio karibu kushinda. Niko nafasi ya 4.
Mtangazaji: Ngoja! Kuna mvurugo mkubwa hapa na kuna ripoti kuwa baadhi ya ngamia wakekunywa dawa za kusisimua misuli. Nambari 3, 27, na 1 wametolewa! Hilo linamfanya nambari 7 kuwa mshindi rasmi!
Kamelia: Kamelot, ulishinda!

Kamelot: Lo!! Bwana asifiwe! Asanti kwa usaidizi wako, Kamelia. Karibu sifa zangu ziharibike, ila sasa najua nilikimbia katika namna iliyo mheshimu Mungu. Lo! Nahisi kiu sana! (Anazamisha pua nyuma ya jukwaa na kunywa mara 1 kidogo.) Aaaah hayo maji yanatosha kwa wiki hii. Sasa nahisi njaa.

## SOMO KUU 1

Karibu katika VBS ambapo tunasoma jinsi ya kuwa jasiri mbele ya Mungu! Zamani za kale, wanaisraeli walichukuliwa mateka na kuletwa Babeli na Mfalme Nebukadneza. Hofu sana! Watu wa Mungu walikuwa wakiishi katika nchi geni ambayo haimjui Mungu. Kwa namna kama hii, tunaishi katika ulimwengu ambapo watu hawamjui Mungu au kujaribu kumfuta. Ila Mungu alikuwa na wanaisraeli huko Babeli na kufanya vitu vizuri; kwa namna kama hii, Yuko nasi sasa katika ulimwengu huu uliovurugika. Kila mtu aseme, “Ujasiri unamwekaa Mungu mbele!”

Je, ushawahi kutusiwa ukiwa shuleni, au kuona mtu akitusiwa? Je, walimu wako washawahi kukufunza mambo ya kumuasi Mungu? Je, watu washawahi jaribu kukushawishi ufanye mambo yasiyofaa? Jambo kama hili lilitendeka Babeli. Mfalme Nebukadneza aliwachukua vijana bora kutoka Israeli na kuwasajili katika chuo kikuu cha Babeli ili kusoma jinsi ya kutumikia huduma ya Mfalme. Walikuwa ni pamoja na Danieli, Mishaeli na Azaria. Kila mtu aseme, “Ujasiri unamweka Mungu Mbele!”

Mfalme aliyabadilisha majina yao, akawafunza dhana zilizokuwa tofauti na amri za Mungu, na akawapa chakula kilichokuwa tofauti. Vijana hawa walikubali kudhihakiwa na wakawaskiza waelekezi wao kwa subira, ila walikataa kabisa vyakula vile kwa sababu ilikuwa ni kukosa kumtii Mungu moja kwa moja. Kwa namna kama hii, ulimwengu unajaribu kutufanya kudanganya, kusema uongo, kuiba, kuwa wakali kwa wengine, au kuabudu vitu vingine bali na Mungu. Mungu ametwambia tusifanye mambo haya na tunafaa kumtii licha ya shinikizo kutoka kwa ulimwengu. Kila mtu aseme, “Ujasiri unamweka Mungu mbele!”

Danieli alikuwa na busara kuhus jinsi alivyokataa. Alimwuliza mwanaume aliyekuwa msimamizi wao kuchunguza vyakula hivi kwa siku 10 ili kuona kama vilikuwa ni bora. Unaweza kumwomba Mungu hekima ya jinsi ya kukataa kushinikizwa na kumtii. Kila mtu aseme, “Ujasiri unamweka Mungu mbele!”

Baada ya chuo kikuu, vijana hawa waliingia katika huduma ya mfalme, kufanya kazi na serikali na usimamizi. Walifanya kazi nzuri sana hadi wakapandishwa vyeo hadi mamlaka makubwa katika ufalme ambapo waliweza kuboresha maisha ya watu wengine. Yesu anasema kuwa sisi tunaomwamini ni mwangaza kwa ulimwengu. Mungu atakuweka mahali ambapo utaweza kuonyesha mwangaza wake kwa ulimwengu, iwapo utaingia katika siasa, biashara, uhandisi au teknolojia, udaktari, kuwatunza watoto nyumbani, michezo, ukasisi, uchungaji, ufunzaji au usimamizi. Mungu atakutumia kuanzia hadi sasa ukiwa shuleni, nyumbani, au katika eneo unakoishi ili kufanya ulimwengu kuwa bora zaidi kwa wengine. Haijalishi utakachokifanya, mweke Mungu mbele na umtii bila kujali lolote. Kila mtu aseme, “Ujasiri unamweka Mungu mbele!”

## UFUNDI KATIKA MILKI 1

*Roho*





### *Nyenzo*


*Utepe uliojikunjakunja, sentimita 50
*Roho ya karatasi
*Bango lililo na Mstari wa Biblia
*Gundi
*Rangi


### *Maelekezo*


* Kata roho na bendera. Zipake rangi kwa kutumia rangi unazozipenda zaidi.
* Kwa kutumia gundi shikanisha peo zote mbili za utepe hadi nyuma ya roho ili kuunda kitanzi. Kwa kutumia gundi shikanisha kipande cha bendera sehemu ya katikati utepe.

## DARASA KATIKA KASRI 1











| | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | L | I | Y | E | B | A | D | I | L | I | S | H | W | A |
| V | U | A | B | N | A | M | A | U | A | Z | N | A | W | K |
| Y | O | H | U | D | B | K | N | V | B | A | F | D | A | U |
| A | N | E | I | K | E | F | I | S | A | D | I | M | Z | F |
| K | G | K | R | F | L | V | E | B | F | B | A | N | A | U |
| U | O | I | I | B | I | A | L | V | A | I | K | V | G | A |
| L | M | M | S | K | U | D | I | H | U | V | B | F | N | T |
| A | D | A | A | N | D | A | N | G | A | N | Y | A | A | A |
| K | B | U | J | U | L | I | M | W | E | N | G | U | W | D |



| | |
|---|---|
| 5 | 1 |
| 14 | 4 |
| 6 | 7 |
| 12 | 11 |
| 8 | 13 |
| 9 | 2 |
| 10 | 3 |



## MASWALI NA MAJIBU 1

1. **Ni mambo gani mabaya yanakaa "SAWA" kwa sababu "kila mtu anayafanya"?**
   Mifano: Kuiba peremende, kutupania taka, kudanganya ili kuepuka adhabu, kupatiana ahadi ambazo huwezi timiza.
2. **Je, mbona chifu wa maafisa wa chumba cha ufalme waliwachagua vijana hawa? Je, Mungu aliona nini ndani yao tofauti na vile watu walivyowaona?**
   Walikuwa wanaisraeli waliokuwa bora na wazuri zaidi. Danieli 1:3-4. Mungu aliwapata kuwa waaminifu kwake. Alikuwa ni yeye ndiye aliyewapatia uwezo wao. Danieli 1:17
3. **Je, Mungu amekupa nini?**
   Mifano: Wagalatia 5:22-23 Matunda ya Roho Mtakatifu, talanta, uwezo, urithi.
4. **Je, "kumweka Mungu mbele" kunafana na nini?**
   Mifano: kutubu na urejesho, kuomba msamaha kwa uliowakosea, kumtii Mungu badala ya marafiki.
5. **Je, hawa watu walikuwa kina nani katika simulizi?**
   Jibu: Mfalme Nebukadineza, Danieli, Hanania, Mishaeli, na Azaria (au Belteshaza, Shadraki, Meshaki, na Abednego)

## KAZI YA ZIADA 1

Fikiria kitu ambacho ni kigumu kutii kwa Mungu. Mwulize Mungu kukupa usaidizi, halafu umtii siku mzima.

## SARAKASI NA DANIELI 1

Mwalimu: Ni jambo la kufurahisha kwamba Danieli ametafuta muda kutoka kwa ratiba yake iliyojaa shughuli kama afisa mkubwa katika milki ili kututembelea na kutusimulia kuhusu maisha yake.

Danieli: Hamjambo, kila mtu. Mimi ni Danieli, na ni vizuri kukutana nanyi wote. Nilifurahia sana wakati msaidizi wangu aliniambia kwamba tulikuwa tumeratibiwa kuwa na mahojiano na darasa lililojaa wanafunzi. Mko na uwezo mkubwa! Hamna habari mambo mazuri ambayo Mungu anataka kuwatendea. Sikuwa na habari ni mipango gani Mungu aliyokuwa nayo kwangu. Wacha tuone… nikiwa mchanga, mimi na marafiki zangu tuliishi Israeli. Tulikuwa watu wa Mungu, ila Wanaisraeli wengi walikuwa wakiabudu miungu isiyofaa ambayo haiwezi kusikia wala kuongea wala kufanya chochote. Nilitoka kutoka kwa familia ya ukuu, na tuliskia habari zote kuhusu mfalme Nebukadneza alivyokuwa akiyateka mataifa mengine mashariki mwetu. Viongozi wa jamii walikaa wakinena kuwa, "Sisi hatutashindwa." Walikuwa wakiwasikiza manabii wa uongo ambao walisema kuwa Mungu angetulinda hata tungefanya lolote na kwamba tungeweza kukosa kutii na kufanya lolote tulilolitaka. Yeremia na wengine wachache walisisitiza kuwa tungeshindwa na Nebukadneza na

kutekwa. Niliwaza kuwa tungekufa au kuwa watumwa… hebu fikiria butwaa iliyoniingia waliponipeleka mimi na baadhi ya wenzangu hadi chuo kikuu cha Babeli! Tulikuwa tusome shahada ya miaka 3 halafu kumtumikia mfalme. Tuliamua kufanya lolote katika kila hali ambayo Mungu alitutia. Ilikuwa ngumu mara nyingine, kama tulibadilisha majina yetu yaliyomtukuza Mungu na kuitwa majina yaliyotukuza miungu isiyofaa, kama jina langu jipya Belteshaza. Mara ya kwanza hata singeweza kulitamka. Na walikuwa na dini geni sana pale shuleni. Ila walipotwambia kula vyakula visivyofaa tuliamua hatungekula. Tuliamua kumweka Mungu mbele licha ya tulipokuwa na kumtii Mungu hata kama ingekuwa ni sisi tu tuliofanya hivyo. Mtu aliyetusimamia alihisi woga kubadilisha vyakula vyetu. Nilimwuliza kukibadilisha kwa siku kadhaa tu, na alifanya hivyo!

Mungu alikuwa nasi na alitusaidia. Tulikuwa wenye afya kuwaliko vijana wengine, na Mungu alitusaidia kufanya vizuri shuleni. Baada ya kuhitimu, tulikuwa na mahojiano ya kazi na mfalme. Ilikaa jinsi hivyo ilivyokuwa wakati familia yangu ilipokwenda kumtembelea Mfalme wa Israeli kwa fahari na itifaki zote zilizofaa, ila itifaki hizi zilikuwa tofauti kiasi na za Babeli. Hata hivyo, mfalme alituchukua katika huduma yake, na tumekuwa tukihudumia milki kutoka wakati huo.

Mwalimu: Je, ulijua kwamba licha ya haya yote ungekuwa afisa mkubwa katika milki?


Danieli: La, sikujua. Usijaribu kuwa mtu mkubwa ila zingatia kumweka Mungu mbele na kufanya kazi kwa uhodari na uadilifu. Watu watatambua, na Mungu pia.

Mwalimu: Asanti sana kwa kuja, Danieli! Najua kuwa uko na ratiba iliyojaa mambo mengi katika kuendesha milki. Tutakutana nawe kesho

## SHUGHULI 1


***Vipaumbele***

Mpe kila mtoto karatasi ya kuchora piramidi kama picha ya mfano na kuwataka kuandika mambo 5 wanayoyapatia kipaumbele katika maisha yao katika Piramidi. Kabla ya kuandika la kwanza, wahimize kumweka Mungu mbele kama kipaumbele. Wakumbushe ni nini Biblia inachosema kuhusu Mungu (Yeye ni mwokozi wetu, mwelekezi wetu, nguvu yetu, na ni mzuri na anatupenda jinsi tulivyo, n.k.) Halafu watoto wanaweza kuendelea kuandika na kujadiliana na wengine mambo wanayoyapa kipaumbele.



## KARAMU YA KIFALME 1

***Taji la Sandiwichi***



***Viungo:***

- Mkate wa boflo
- Karatasi
- Kisu
- Kuweka chaguo lako la kijazio (Hemu, mboga, au jemu)

*Maelekezo:*

1. Tengeneza kalibu ya karatasi iwe taji.
2. Tengeneza sandiwichi kwa vipande viwili vya mkate na mshindilio wako
3. Weka taji hili la karatasi juu ya kalibu na kuikata sandiwichi.

***Tayari! Sasa tunaweza kufurahia karamu yetu ya kwanza ya kifalme!***

# MICHEZO YA BUSTANI 1

### *Kuwa mwangaza wa ulimwengu*



Gawanya darasa kuwa timu mbili. Ficha taa inayowaka chini ya kitu kizito ambacho hakikubalishi mwangaza kupenya (kwa tahadhari ya moto). Halafu, zima taa kuu ya chumba na kumwambia mtoto kutoka kila chumba kwenda kutafuta taa iliyofichwa. Rudia mchezo huu ili kuwapa watoto wengine fursa ya kucheza. Fafanua kuwa Yesu Kristo alitwambia kuwa sisi ndio mwangaza wa ulimwengu, na kwamba hatufai kuuficha mwangaza huu ila tunafaa kuendelea kumtii Mungu katika kila hali. Tunafaa kuwa jasiri kwa Mungu!

### *Ngamia Inasema…*



Mwalimu au mtoto atachukua fursa na kuwa “ngamia.” Huyu mtu ataongoza kila mtu katika utendaji, kwa mfano, kuzunguka, kuruka kwa mguu mmoja, au kutoa sauti anayotoa ngamia. Akisema “Ngamia anasema…” kabla ya utendaji, watoto wengine wote ni lazima wafanye tendo au watolewe katika mchezo. Iwapo hataanza na “ngamia anasema…” basi watoto wengine wote hawafai kufanya tendo, na yeyote atakayetenda atatolewa katika mchezo. Wape watoto kadhaa fursa ya kuwa ngamia. Fanya maelekezo kuwa haraka zaidi ili kuifanya kuwa burudani.

# 2. UJASIRI UNAMWAMINI MUNGU

## Danieli 3: Jaribio la Moto

### VIMAKINISHI / MAKOFI 2

"Ujasiri ni kumwamini Mungu"

1. "Ujasiri" = Kunja ngumi halafu mgonge rafiki kwa ngumi
2. "Ni kumwamini" = Mgonge kwa ngumi juu halafu tena chini
3. "Mungu" = Nyoosha kuelekea mbinginu kwa upande mmoja kwa mikono yote miwili

### MSTARI WA KUMBUKUMBU 2

*Zaburi 47:2 "Kwa kuwa BWANA Aliye juu, mwenye kuogofya, Ndiye mfalme mkuu juu ya dunia yote."*

### SARAKASI 2: NGAMIA VITANI

Kamelot: (Kwenda kama askari mbele na nyuma katika jukwaa) Hut! 2, 3, 4, Hut! 2, 3, 4…
Kamelia: Je, unafanya nini?
Kamelot: Naneda kama askari. Je, hujawahi kuona watu wakienda kama askari?
Kamelia: La sio hivyo unavyofanya
Kamelot: Basi, wanasajili kitengo kipya cha ngamia hivi leo. Kwa sababu, farasi za adui zinashtuliwa na mnuko wetu.
Kamelia: Lo hapana, unanuka sana hadi ni lazima wakusajili!
Kamelot: Najua, ila sitaki kwenda katika vita. Yaani, nataka kulisaidia taifa langu, ila pia sitaki kumwumiza mtu yeyotel Sijui nitakalolifanya! Basi…. Kawaida sana.
Kamelia: Je, utafanya nini?
Kamelot: Nilikuwa nafikiria kuburuka, ila naogopa urefu kutoka juu. Oh, naweza kujificha ili wasinipate. (anatumbukiza kichwa kiasi chini ya pazia la jukwaa kwa namna kichwa chake na maskio yake yanaonekana.)
Kamelia: Um… Bado nakuona.
Kamelot: Ni lazima uwe na maono ya eksirei. Naweza kujifanya kuwa… tausi! (Shika mkono wa shabiki mmoja nyuma ya Kamelot)
Kamelia: Tausi mkubwa, mwenye nywele, asiyependeza.
Kamelot: Lo! Hilo sio jambo nzuri kusema kuhusu tausi! Haya, halitumiki. Siwezi fikiria njia ya kulitoa kwa akili.
Kamelia: Unaweza kumwomba Mungu kukupa usaidizi! Hata ingawa haufikirii namna, anaweza.
Kamelot: Mpenzi Mungu, tafadhali nisaidie na uniokoe! Haijalishi litakalotendeka, nakuamini. Oh, ni wakati. Naweza kwenda. (Anatoka jukwaani)
Kamelia: Ndio, Mungu, tafadhali msaidie.
Announcer: Muda mfupi unapita…
Kamelot anaingia katika jukwaa: Lo, hiyo ilikuwa ni vita kali!
Kamelia: Ulikwenda vitani? Nilidhani Mungu hangekupeleka vitani.
Kamelot: Kweli,mimi pia. Ila inakaa kuwa nanuka sana kwa hivyo hakuna mtu angenikaribia, kwa hivyo hakuna mtu niliyemwumiza!
Kamelia: (Anacheka kiasi ila anajaribu kuacha) Pole. Hilo sio jambo la kuchekesha, ila inafurahisha kuwa lilikusaidia!
Kamelot:Kwa sababu hakuna aliye kuwa karibu sana ili kupigana, tulizunguka tu tukiwaokoa watu. Mvulana mmoja alikuwa amezirai. Mvulana mwingine alijidunga kidole sana kwamba ilibidi ashonwe.
Kamelia: Woah, hivyo ni vibaya. Siwezi kufikiria kudunga kwato zangu hivyo sana. Je, ni nini hiyo uliyoivaa?
Kamelot: Walinituza medali kwa kuwaokoa watu. Hata hivyo, nafurahia kuwa vita vimeisha. Chakula kilikuwa kizuri, ila natamani nafaka za nyumbani. Na hivyo kusema, nahisi njaa sasa.

## SOMO KUU 2

Karibu sana katika VBS, ambapo tunasoma jinsi ya kuwa jasiri mbele ya Mungu. Wakati uliopita tulisoma jinsi ya kuwa watiifu kwa Mungu licha ya shinikizo. Leo tutasoma ni nini kinachofanyika baada kukataa kushinikizwa. Mfalme Nebukadneza aliunda sanamu ya dhahabu na kuwaambia maafisaa wake kwamba ni lazima wangeabudu mungu huyu. Mungu alisema tunafaa kumwabudu na kumtukuza Yeye pekee. Pia, marafiki zetu, Shadraki, Meshaki na Abednego (mfalme aliyabadilisha majina yao kutoka Hanania, Mishaeli, na Azaria) walikataa kushinikizwa na kukataa kukosa kumtii Mungu. Kila Mtu aseme, "Ujasiri ni kumweka Mungu mbele!"

Mfalme aliwapa fursa moja ya mwisho, na kuwatisha kuwatupa kwenye moto mkubwa iwapo hawangeabudu sanamu ile. Walisema, "Mungu wetu anaweza kutuokoa. Ila hata asipotuokoa, hatutaabudu sanamu hii." Mungu wetu ndiye mkubwa sana, na ndiye mwenye nguvu sana katika ulimwengu, na tunafaa kumtii. Mungu pia anatuahidi kututuza mbinguni kwa milele kwa tunayomfanyia hapa ulimwenguni. Mungu ndiye pekee tunafaa kuogopa, ila anatupenda na ana nguvu ya kutuokoa kutoka kwa jambo lolote, hata kifo! Shadraki, Meshaki na Abednego, walitambua hili na kuamini na kujipa kwa Mungu ili awaokoe kwa namna yoyote aliyoitaka, iwapo hapa ulimwenguni au mbinguni. Kila mtu aseme, "Ujasiri ni kumwamini Mungu!"

Mfalme Nebukadneza alijawa na hasira nyingi na aliagiza tanuri kutiwa moto ili liwe moto mara saba zaidi, na akaagiza Shadraki, Meshaki, na Abednego kutupwa kwenye tanuri. Mara nyingine tunafikiria kuwa Mungu anaweza kutatua hali zetu ngumu kama vile, mtu anayetunyanyasa shuleni, kutoelewa masomo, mzazi kupata kansa, ama uhamiaji katika jiji jingine. Mara nyingine, anatusaidia, na tunafaa kumwomba usaidizi. Katika simulizi hii, hakuwatoa kwenye tanuri, ila bado walimwamini. Wacha tuone nini kilichofanyika! Kila mtu aseme, "Ujasiri ni kumweka Mungu mbele!"

Nebukadneza alishtuka, aliona wakitembea ndani ya moto wakiwa hawachomeki na walikuwa pamoja na mtu mwingine wa nne ambaye alisema alifanana na "mwana wa miungu." Mungu alikuwa nao ndani ya moto wa tanuri! Kwa hivyo, pia tunapojipata katika hali ngumu, Mungu atakuwa nawe katika hali hizi. Mungu alituahidi kuwa hatawai tuacha au kutusahau. Kusema kweli, Mungu yupo karibu nasi sana zaidi katika hali ngumu kuliko hali za furaha, na anazitumia kuonyesha nguvu zake katika maisha yetu. Ona jinsi Mungu anavyotupenda! Kila mtu aseme, "Ujasiri ni kumweka Mungu mbele!"

Shadraki, Meshaki, na Abednego walitoka nje ya moto wakiwa hawajachomeka hata kiasi wala kunuka moshi. Kwa usaidizi wa Mungu, unaweza kutoka katika hali ngumu bila uchungu, hasira, woga, au chuki ila kama umejawa na upendo wa Mungu, furaha, amani na msamaha. Mfalme Nebukadneza alitambua kuwa Mungu wetu ndiye mkuu. Siku moja Yesu atarudi, na ulimwengu wote utapiga magoti mbele ya Yesu Kristo kuwa yeye ndiye mfalme wa ulimwengu wote.

Dhambi zetu, kila kosa tunalofanya linatutenganisha na mungu. Yesu alituokoa kutoka kwa dhambi zetu aliposulubishwa kisha akafufuka. Yeyote anayemwamini Yesu ataokolewa milele, ila yeyote ambaye hamwamini Mungu hataokolewa. Je, utaweka imani yako kwa Yesu leo na kumwomba kukuokoa kutoka kwa dhambi zako na kuwa Mungu wa maisha yako milele? Omba: "Yesu Mungu, najua kwamba wewe ndiye mfalme wa ulimwengu wote. Yesu, ningeomba utusamehe dhambi za maisha yangu? Nakuamini kuniokoa milele."

## VIFAA KATIKA MILKI 2

*Tanuri*




***Nyenzo***


*Utako wa Karatasi ya tanuri
*Maumbo ya moto wa Karatasi
*Rangi
*Gundi


***Maelekezo***

* Kata tanuri na moto. Paka rangi katikati ya tanuri na moto na watu (kumbuka kuwa watu hawa hawakuumia).
* Paka rangi moto na rangi ya machungwa, manjano,na nyekundu ili kufanana na moto.
* Kunja kingo za pande za moto na uzitie gundi na kuzibandika katika tanuri ili zifunguke kama moto.

## DARASA KATIKA KASRI 2












| | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | A | L | I | M | I | S | H | A | Z | A | U |
| H | U | K | M | O | T | D | Z | Y | M | S | J |
| A | O | T | U | S | N | I | K | T | N | U | A |
| D | K | M | I | H | U | R | U | N | A | T | S |
| R | O | U | S | I | A | Y | I | N | A | M | I |
| A | Z | F | G | A | Y | M | K | A | B | U | R |
| K | I | U | U | D | L | E | Z | M | E | N | I |
| A | S | F | K | S | I | A | S | Y | D | G | M |
| O | M | U | T | Y | S | D | B | U | N | U | K |
| T | A | O | G | I | A | U | G | A | E | S | U |
| O | Y | M | A | D | U | Z | T | S | G | A | T |
| M | E | S | H | A | K | I | K | I | O | Y | I |





## KAZI YA ZIADA 2

Kumbuka mida yoyote unapofikiria kuhusu Mungu kuwa nawe leo na kumwambia mwalimu kesho.

## MASWALI NA MAJIBU 2

1. **Je, adhabu ya kukosa kuabudu sanamu ya moto iliyoundwa na mfalme ilikuwa ni gani?**
   Adhabu ilikuwa kutupwa ndani ya tanuri ya moto mkubwa.
2. **Je, iwapo Mungu hatawaokoa Wakristo kutoka kwa shida, hili linaonyesha nini?**
   Kuna majibu kadhaa yanayowezekana: Jaribu la imani, kuonyesha nguvu zake za uokozi, kumtambua akiwa nasi katika shida, kuwa ushuhuda kwa wengine wa imani yetu.
3. **Je, ni mashida gani yanayoweza kufanya Mungu kukuacha?**
   Waebrania 13:5 "Sitakuacha kamwe, wala sitakutupa."
   Dhambi zinatutenganisha na Mungu, ila kupitia kwa Yesu, tunaridhiana na Mungu. Ili kumhisi kuwa nasi kila wakati, licha ya shida tunazopitia, ni lazima tumkubali Yesu kama mwokozi wetu.
4. **Je, nani alikuwa ndani ya moto huu mkubwa?**
   Shadraki, Meshaki, Abednego, na Mungu = 4. Hakukuwa na simba wowote.
5. **Je, unaweza kuokolewa aje?**
   Unaweza kuomba: "Mungu baba, najua kwamba wewe ni mfalme wa ulimwengu wote. Je, Yesu, utanisamehe dhambi zangu na kuwa Mungu wa maisha yangu? Nakuamini kuniokoa milele."

## SARAKASI NA DANIELI 2

Mwalimu: Karibu tena, Danieli!

Danieli: Asanti. Nafurahi sana kurudi hapa, na nasisimuka kuongea kuhusu Mungu wetu mkuu na simulizi za kushangaza na marafiki zangu. Shadraki, Meshaki na Abednego. Nakumbuka kuwa hiyo siku walikuja wakitetemeka kwa furaha. Mfalme Nebukadneza alijenga sanamu kubwa sana na aliwataka maafisaa wa serikali kuiabudu katika sherehe ya uwakafu. Oh, iwapo tu watu wangetambua kuwa sanamu haiwezi kuwa mungu kwa sababu haiwezi kuona wala kuongea au kufanya lolote. Ila watu kote katika historia wamekuwa wakiabudu vitu vidogo sana.

Marafiki zangu walikataa kuabudu sanamu. Walitumai hawangeshikwa, ila watu fulani walimwambia mfalme. Tulikuwa tofauti na watu wengine waliotuzingira, na hawakutupenda kwa sababu hii na mara nyingine walitaka kutuumiza. Usijali hata ingawa watu wanaokuzingira hawakubaliani nawe katika unachokifanya. Unafaa kuamua ni kauli gani unafaa kuijali, hasa kama mtoto au kijana. Chagua vinavyofaa unaopitisha muda nao. Ninashukuru Mungu kwa marafiki zangu Shadraki, Meshaki na Abednego. Tumekuwa tukihimizana kila wakati kumtii Mungu, na ninafurahishwa sana na ujasiri wao. Mara nyingine, wanahitaji kutiwa moyo nami na mara nyingine wananitia moyo. Jaribu kutafuta marafiki kama hao. Basi, walioshikwa, adhabu ilikuwa ni kutupwa katika tanuri ya moto mkubwa! Walipokataa na kumwamini Mungu na maisha yao licha ya lolote, Mfalme aliingiwa na hasira kubwa na akaagiza moto kuongezwa hata zaidi hata uliwaua waliowatupa marafiki zangu katika tanuri.


Ila marafiki zangu waliishi! Nilishtuka sana waliponiambia simulizi hii, kwa sababu hawakuchomeka. Hawakukuwa na moshi au nywele au nguo zilizochomeka. Hili lilishtua mfalme pia. Aliabudu Mungu na kutambua kuwa Mungu wetu ndiye Mungu mkuu sana anayesimamia vitu vyote. Nafikiria kitu kizuri sana ni kuwa kulikuwa na mwanamme wa nne

ndani ya moto. Mfalme alisema kuwa alifanana na “mwana wa miungu.” Sijui kwa uhakika kama alikuwa ni malaika ama ilkuwa ni nani, ila ni dhahiri Mungu alikuwa nao katika moto. Natamani ningekuwepo hapo ili nione jinsi ilivyokuwa. Siku moja, nitapata kumwona Mungu mbinguni. Hata hivyo, ninafuraha kuwa na marafiki jasiri na wanaomwamini Mungu. Mfalme na kila mtu mwengine wanapenda sana wanapoona jinsi marafiki wangu wanavyomtii Mungu. Inawafanya kuhisi kana kwamba kuna kitu wanachokosa. Nani ajuaye? Labda wengine wataanza kumwabudu Mungu wetu na kuacha kuabudu vitu vidogo.

Mwalimu: Je, ni ukweli kwamba wangekuwa “SAWA” iwapo Mungu hakuwaokoa ndani ya tanuri?
Danieli: Ndio, hicho ndicho kiwango walivyojitolea marafiki zangu. Tunajua kuwa tutakuwa na Mungu siku moja mbinguni. Ningetaka sana kuwaona, ila najua siku moja tutakuwa pamoja. Ila badala yake Mungu aliamua kuwaokoa kwa namna hii, na Mfalme aliamuru kila mtu katika milki kutosema jambo lolote kumhusu Mungu. Mungu wetu ni mkuu, na ataabudiwa na kila mtu.
Mwalimu: Asanti tena kwa kuja tena, leo.

## SHUGHULI 2

*Naamini*



Kikundi kinaunda mduara. Mtu mmoja anaanza kwa kusema “Namwamini Mungu kila kunapokucha." Mtu anayefuata anasema, “Namwamini Mungu kunapokucha na babangu anacheka." Kila mtu anarudia orodha hii na kuongeza jambo jingine moja. Lengo ni kuweza kukumbuka vitu vyote ambavyo watu wengine wamesema kabla yako.

“Iwapo kuna wakati,cheza tena kwa kusema kinyume.” “Namwamini Mungu hata nisipoiona siku ingine, au baba yangu hajacheka."

## KARAMU YA KIFALME2

*Moto wa Matunda*



***Viungo:***

- Zabibu
- Matunda ya manjano au rangi ya machungwa au mboga (Embe, Nanasi na / au karoti)
- Pretseli (au kitu kingine kinachofanana na kuni)
- Kisu
- Sahani



***Maelekezo:***

1. Kata tunda hili la manjano kwa namna ya miali ya moto (miiba)
2. Weka tunda hili katika sahani pamoja na zabibu zikiizingira ili kufanana na mawe.
3. Ongeza pretseli au vyakula vilivyokangwa ili kufanana na kuni.

***Tayari! Tunaweza kufurahia moto wetu bila kuchomeka!***

***Ila tusisahau kwamba... jinsi tu Mungu alivyokuwa nao ndani ya moto, pia Yuko nasi katika hali ngumu!***


# MICHEZO YA BUSTANI 2



## Densi ya Ngamia

Cheza mziki na kuwaambia kucheza densi kama ngamia. Unaweza kuwaonyesha video ya ngamia ikicheza densi ili wajue jinsi ya kufanya hivyo. Unapozima mziki, watoto wote wanafaa kukaa ni kama wamegandishwa. Mtoto atakayetoka kwenye mchezo atatakiwa kuketi chini. Cheza mziki tena na kuurudia tena hadi kuwe na mshindi mmoja.

## Mchezo wa kuvuta kamba



Katika mchezo huu utahitaji kamba nzito sana ambayo haitawaumiza watoto mikono. Unda timu kulingana na nambari ya watoto waliopo (kama vile timu 4 au 6). Timu mbili zinacheza wakati mmoja, kujaribu kuvuta upande wao wa kamba ili eneo la katikati mwa kamba liwe katika eneo lililotiwa alama katika sakafu. Shindaneni hadi kuwe na timu itakayoshinda.

# 3. UJASIRI NI KUSEMA KWELI

## Danieli 4: Ndoto iliyokuwa na habari mbaya

## VIMAKINISHI / MAKOFI 3

"Ujasiri ni kusema kweli"

1. Weka mikono kinywani kama kipaza sauti
2. Sogeza kichwa kwa namna ya duara huku ukisema"Eeeeeh ooooh"
3. Sogeza mikono kwa namna ya Hip Hop huku ukisema, "Unaweza kutusikia?"

## MSTARI WA KUMBUKUMBU 3

*1 Wakorintho 13:6 "haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli."*

## SARAKASI 3: NGAMIA ANACHEZA DENSI

Kamelia: Kamelot!! Saidia, Kamelooot!!

Kamelot anaingia katika jukwaa kwa haraka: Nini!? Nini?? Je, kuna buibui? Je, kuna hayawani mkubwa aliyetoka baharini? Je, uko wapi moto? Nitautemea mate! (anajitayarisha kuutemea mate)

Kamelia: La, la. Kuvaa viatu vyangu vya kucheza densi (Chukua viatu vya wasichana)

Kamelot: Je, mbona nivae viatu vyako?

Kamelia: La, sio wewe. Ni mimi! Ni wakati wangu wa kuigiza.

Kamelot: Kuigiza? Hukuniambia kuhusu maisha yako ya zamani ya ajabu kama mwanasarakasi au mwimbaji wa opera?

Kamelia: Niko katika mashindano ya kucheza densi ya ngamia, ndiyo! Nafurahia sana. Ugumu upo kunyoosha vidole vyangu vya mguu juu ya jukwaa.

Kamelot: Hapa, wacha nijaribu. (Anaruka juu na chini kiasi, halafu anajitega na kuanguka nyuma ya jukwaa) Aaah! *Mgongano*

Kamelia: Ona? Ni vigumu! Ila naweza lifanya kwa sababu najua sana kucheza densi. Hata sio lazima nifanye mazoezi kwa sababu niko na talanta kuu. Nilifika kiwango hiki cha ushindani kivyangu.

Kamelot: Kuringa kwako sio kuzuri.

Kamelia: Lakini ni kweli!

Kamelot: Ukweli ni kwamba Mungu alikupa talanta uliyo nayo, na mmiliki wako alikusaidia kufanya mazoezi na kujiimarisha katika mashindano mengine.

Kamelia: Tazama tu. Nashinda mashindano haya virahisi.

Kamelot: Nitaleta tishu. Na bendeji kiasi!

Kamelia anatoka kwa haraka.

Announcer: Baada ya mashindano…

Kamelot amelala na anang'orota.

Kamelia anaingia huku akilia kwa sauti kubwa.

Kamelot: Nini mbaya? (Anampa Kamelia kitambaa cha mkono)

Kamelia: (Anatoa kamasi kwa tishu. Akilia, kwa sauti kubwa…) Sikushinda! Majaji hawakufanya maamuzi yaliyo sawa. Nilifaa kushinda. Nilifaa kushinda! Ngamia huyo mwingine alianguka mara mbili! Na utaratibu wangu ulikuwa mzuri ! Basi, Nilianguka mara tu moja … ndiyo, labda mara 3. 4. (kupumua) 7. Ila bado, Nilifaa kushinda!

Kamelot: Kwa hivyo, ulianguka mara 7 na unafikiria kuwa bado ulifaa kushinda? Basi ningeanguka mara 100 na kushinda!

Kamelia: Wewe! Mi--- Basi— La, hili ni tofauti kwa sababu-- Oooohhh. Unasema ukweli. Majaji walifanya uamuzi ulio sawa. Nilifanya vibaya tu na kupoteza! (Analia tena, kwa sauti kubwa)

Kamelot: Unalia kana kwamba unaringa na bado unajihurumia, Kamelia. Hapa, wacha tufikirie ukweli tena.

Kamelia: (Anapumua) Unamaanisha nini?
Kamelot: Sema hili nami. Ukweli ni ati mimi ni wa Yesu. Uwezo wangu unatoka kwa Mungu. Alinipatia uwezo huu, na anaweza kuuchukua kwa urahisi tu jinsi alivyonipatia… ila hakuna kitu kinabadilika, thamani yangu au kiwango cha upendo wake kwangu. Sitateta kuhusu kilichofanyika ila nitajifundisha kutoka kwa jambo hili na kumwomba Mungu anipe usaidizi ili kufanya vyema wakati mwingine.
(Kamelia anarudia pamoja na Kamelot)
Kamelot: Unajihisi vizuri?
Kamelia: Ndiyo, kiasi.
Kamelot: Vizuri, kwa sababu nilikuwa nimelala kidogo … Ila sasa… Nahisi njaa!

## SOMO KUU 3

Karibu tena katika VBS! Kumbuka, ujasiri unamweka Mungu mbele na kumwamini Mungu. Sasa kila mtu aseme, “Ujasiri unamweka Mungu mbele!”

Mfalme Nebukadneza aliota ndoto kuhusu mti mkubwa ambao ulileta kivuli na kutunza ulimwengu mzima. Halafu mti huu ukakatwa, na mjumbe alisema akasema kuwa angekula nyasi na kwamba nywele na kucha zake zingekua ndefu. Mfalme alimwita rafiki yetu Danieli kumfafanulia, kwa sababu kila mtu alijua kuwa Mungu alikuwa na Danieli. Mungu alifichua maana ya ndoto hiyo kwa Danieli, na ilimaanisha kuwa mfalme angetokwa na wazimu na kudhani yeye ni mnyama. Je, ungefanya nini? Je, ungedanganya na uongo mzuri au ungesema ukweli? Kila mtu aseme, “Ujasiri unasema ukweli!”

Danieli alimwambia mfalme ukweli kuhusu habari hizi mbaya. Sio hivyo tu, ila kwa heshima alipendekeza kuwa mfalme alifaa kutubu. Yesu alikuja na neema na ukweli, pia. Aliwapenda watu sana hadi akakabiliana na dhambi na kamwe hakusema kuwa dhambi ni SAWA. Halafu Yesu akatuokoa kwa Kusulubishwa msalabani, na anatuomba kumwamini na kutubu na kubadilisha tunachokifanya. Kwa namna hii, tunafaa kusema ukweli kwa wengine kwa upendo. Kila mtu aseme, “Ujasiri unasema ukweli!”


Mwaka mmoja baadaye, mfalme aliangalia kasri lake na kusema kuwa alikuwa amelijenga kwa nguvu zake na kwa sababu yake binafsi. Ilikuwa rahisi kuingia katika mtego wa kiburi ulipopita mtihani shuleni, kusifiwa na watu, kuishi katika nyumba kubwa, kufanya vizuri katika michezo, au kufanikiwa katika kitu chochote. Kiburi kinasema kwamba ni kwa uwezo wako, ila ni Mungu aliyekuwezesha. Kiburi kinafikiria uko na uwezo, ila ukweli ni kwamba Mungu anaelekeza maisha yako yote. Kiburi kinafikiria mafanikio ni yako, ila ukweli ni kwamba ni ya utukufu wa Mungu na manufaa ya wengine. Kila mtu aseme, “Ujasirii unamweka Mungu mbele!”

Baada tu ya mazungumzo haya yake ya kiburi, mfalme aliingiwa na wazimu! Aliishi nje na kula nyasi kama ng’ombe na nywele na kucha zake zikakuwa ndefu. Baada ya muda mrefu, mfalme aliangalia juu mbinguni na kusema kweli: kwamba Mungu ndiye mwenye nguvu kuu kwa wakati wote. Inaweza kuogofya kukubali kuwa hatuyaendeshi maisha yetu na kwamba maisha sio kwa ajili yetu. Kila mtu aseme, “Ujasiri unasema ukweli!”

Baada ya mfalme kutambua uwezo na nguvu ya Mungu, alirudishwa katika kiti chake cha ufalme, na milki yake ikakua, na akakua mwenye nguvu zaidi. Kisha mfalme akafanya kitu kilichoshangaza. Mfalme aliyekuwa na nguvu sana ulimwenguni aliwaandikia watu wote barua na kusambaza simulizi kuhusu udahifu wake na kumwabudu Mungu wetu mwenye nguvu! Mungu anapofanya kitu katika maisha yako, waambie watu wote kuhusu jambo hili hata ingawa ukweli unakufanya ukae mbaya. Mungu atasifiwa na atakutuza kwa jambo hilo milele, na simulizi yako inaweza kuwanufaisha wengine pia. Katika kitabu cha Ufunuo tunasoma kuwa tunamshinda adui kwa damu yake Yesu na kwa ushuhuda wetu ila sio kwa kupenda maisha yetu. Tunashinda kwa kusema ukweli. Kila mtu aseme, “Ujasiri unasema ukweli!”

## VIFAA VYA MILKI 3

### *Kofia ya Kibabeli*




***Nyenzo***


*Kiolezo cha Karatasi
*Rangi
*Gundi
*Utepe uliojikunjakunja, 50 sentimita

**Maelekezo**

*Kata kiolelezo cha kofia. Paka rangi.
*Kunja katika mistari iliyo na nukta na kuifanya kofia kujilalia kidogo kana kwamba ni vipande 3 tofauti.
*Shikanisha utepe uliojikunjakunja katika mashimo yaliyo katika kila upande na kuifunga kichwani.
*Irembeshe na vimetameta.


## DARASA KATIKA KASRI 3

















## MASWALI NA MAJIBU 3

1. **Je, mbona Nebukadneza alimwuliza Danieli maana ya ndoto yake?**
   Kila mtu alijua kuwa Mungu alikuwa na Danieli. Danieli alikuwa ameonyesha kuwa alimwamini Mungu.
2. **Je, washauri wengine wangemwambia mfalme nini ambacho kingekuwa ni maana iliyofurahisha kwa ndoto yake?**
   Mifano inayowezekana: Mti unaleta kivuli, ulinzi kutoka kwa jua kali na kutoka kwa shida.
   Kula nyasi kunaweza kuwa kula lishe bora na kuwa mwenye afya. Kumea kucha ndefu kunaweza kumaanisha maisha yasiyo na hofu. Kwamba habari za hofu katika ndoto zingemtendekea mtu mwingine ila sio yeye.
3. **Je, uko na nini kilichotoka kwa Mungu?**
   Kubali majibu yote kutoka kwa wanafunzi, pendekeza talanta na sifa, urithi.
4. **Je, mwisho kabisa mfalme alitambua nini?**
   Kuwa Mungu ndiye mwenye nguvu sana kila wakati.
5. **Je, ni kwa namna gani nguvu na mamlaka ya Mungu yanafanana au kutofautiana na ya serikali yako?**
   Mamlaka juu ya jeshi… Mungu ako na malaika, serikali iko na jeshi. Mungu ako na amri ambazo tunaweza kuchagua kufuata. Serikali iko na amri ambazo tunafaa kufuata. Tunapopatwa katika makosa, serikali inaadhibu watu, kama jela, Mungu alitutumia Mwana Wake, Yesu kutuokoa kutoka kwa makosa yetu ili tusiadhibiwe. Mara nyingine serikali zinabadilika: Mungu habadiliki. Mpango wa siku za usoni wa Mungu ni tuishi naye mbinguni, serikali haiwezi kufanya lolote kwa siku zetu za usoni.

## KAZI YA ZIADA

Epuka kusema neno “Mimi” kwa muda wa siku uliobakia. Kila wakati unapohisi kusema neno “Mimi” jiambie kuwa “sio kwa ajili yangu,” na badala yake kuwalenga wengine.

## SARAKASI NA DANIELI 3

Walimu: Karibu tena, Danieli!

Danieli: Asanti. Ni vizuri kurudi hapa. Leo, niko na simulizi nyingine ya kusisimua. Nilikua nafanya kazi katika usimamizi wa serikali siku moja ambapo mfalme Nebukadneza aliponiita. Alikuwa ameota ndoto ambayo alihisi itakuwa ukweli. Mungu alikuwa amenisadia kufafanua ndoto ya mfalme hapo mbeleni. Wachawi na warogi walishindwa kuifafanua tena

mara hii, aliniita. Alisema nilikuwa na roho ya miungu ndani yangu. Haelewi sana kuhusu Mungu, ila anatambua kuwa Mungu yupo nami. Aliniambia ndoto yake ambayo ilihusu mti mkubwa ambao ulileta kivuli katika ulimwengu mzima, na jinsi ulivyokatwa na kufungwa kwa chuma na shaba, na kuhusu amri ya mjumbe kutoka mbinguni aliyesema angeishi nje na kula nyasi na kuwa na akili ya mnyama. Kama alivyoniambia, Mungu alinipatia ufafanuo na nikaelewa kuwa ilikuwa ni habari mbaya kwa mfalme, kuwa angepoteza akili yake, angetokwa na wazimu huku akifikiria yeye ni mnyama na kuishi nje kwa wakati kabla ya kurudishwa katika ufalme.

Mwalimu: Hilo lilikuwa jambo la kushtua kwa mfalme. Je, alikukasirikia?

Danieli: Kweli, ilikuwa ya kushtua. Nimepata imani nyingi miaka ilivyopita, ila ilikuwa ni hatari bado. Lakini nilijua kuwa kitu kizuri kwake ilikuwa ni kumwambia ukweli ili kumpa fursa ya kutubu. Nilipendekeza awache dhambi zake na kuwa mtu mzuri kwa waliodhulumiwa. Mwaka mzima ulipita na kila mtu alikuwa amesahau kuhusu haya yote ambapo mfalme mara moja alitokwa na wazimu. Sikuwa hapo kusikia jinsi alivyotokwa na wazimu, ila aliandikia ufalme wote barua na kueleza kila kitu. Alikuwa amejivuna sana jinsi alivyokuwa amejenga ufalme na kuwa ufalme ulikuwa ni wake. Baada ya muda mrefu, alirudi mwenye afya na mwenye akili timamu, na mara moja tu akarudi katika ufalme. Kisha akaandiikia ufalme wote barua huku akieleza haya yote.

Mwalimu: Aliambia ufalme jinsi alivyokuwa ametokwa na wazimu? Lo, alikuwa amepoteza heshima nyingi.


Danieli: Alifurahiswa sana na Mungu wangu na hata hakujali kuhusu hilo. Unapotambua nguvu ya Mungu, kauli Yake inakuwa kitu pekee unachokijali. Alisema ukweli na hakuficha kitu na alimwabudu Mungu mwenye nguvu zote, na kutambua kuwa Mungu ndiye msimamizi mkubwa wa falme zote katika ulimwengu. Jambo hili lilitutia moyo kama Wayahudi katika milki yote, kuona Mungu akifanya kazi hapa, hata tulipokuwa tumetekwa. Mara nyingine tunafikiria tunafaa kumtetea Mungu au anaweza kutenda tu kupitia maisha yetu, ila anafanya jambo kama hili na kujitetea yeye mwenyewe, na kutuacha tumeshangaa.

Mwalimu: Asanti, Danieli kwa kuja kuwa nasi tena leo. Kesho Esta atakuja kututembelea, ila tutakuona baada ya siku kadhaa, au sivyo?

Danieli: Ningependa sana kuwa hapa ili kusikia simulizi ya Esta, ila natumai nitakuja kuwa nanyi baada ya siku mbili.

## SHUGHULI 3


***Kifaa cha kusema ukweli***



Watoto wakae katika mduara au nusu mduara. Kifaa kinapitishwa katika mduara huu. Mtoto anayepokea kifaa ni lazima aseme ukweli kuhusu maisha yake (Kwa mfano: sipendi kula ndizi kwa sababu ya yanavyokaa) mtoto huyu anafaa kuendelea kusema ukweli kujihusu hadi jirani yake aamue kuchukua kifaa hiki. Wacha kifaa kizunguke na usikubali fursa ya mtu ipite muda wa dakika mbili.

## KARAMU YA KIFALME 3

***Mti kutoka ndoto ya mfalme***



Viungo:

- Ndizi
- Tunda la rangi ya kijani / au mboga (tango iliyokatwa au letusi)

Zaidi:

- Hemu
- Kipande cha karoti

Maelekezo:

1. Tia ndizi katika sahani ili ifanane na gogo la mti.
2. Ongeza tunda la kijani juu ili lifanane na majani ya mtu mkubwa.

Zaiidi:

1. Tengeneza mikunjo miwili ya hemu na uiweke jinsi itakavyokaa mabawa ya kipepeo
2. Weka kipande cha karoti huku kikikaa mwili wa kipepeo.

***Sasa furahia mti kutoka ndoto ya mfalme!!***

## MICHEZO YA BUSTANI 3

### *Kiazi moto*



Unda mduara mkubwa kwa watoto wote, au mmoja kwa wavulana na mwingine kwa wasichana. Wape puto, mpira, au kifaa chochote kwa kila watoto 15 ili kumaliza mchezo haraka zaidi. Unapoanzisha mziki, watoto watapitisha vifaa hivi haraka kwa wenzao katika upande wa kulia na nia ya kutokuwa navyo katika mikono yao kwa muda mrefu. Mziki unapozima, watoto walio na vifaa kwa mkono watatolewa katika mchezo. Cheza kwa haraka hadi kuwe na mshindi tu mmoja.

### *Uso wa Biskuti*



Wachague watoto kadhaa kucheza katika eneo mliloko na kuwapa kila mmoja biskuti. Mchezo utaanza kwa kuweka biskuti juu ya kichwa. Mchezo utakapoanza, mchezaji anapitisha biskuti hadi kinywani kwa kutumia misuli ya usoni mwake.

Iwapo biskuti itaanguka, mchezaji anapoteza mchezo. Kila mchezaji yuko na dakika moja kwa kila biskuti. Yeyote atakaye fanikiwa kupeleka biskuti mbili katika mdomo wake chini ya dakika mbili atakuwa mshindi.

## VIMAKINISHI / MAKOFI 4

"Ujasiri unawaweka wengine mbele"

1. Pamoja na mwenzi, pigeni makofi kwa mikono yenu ya kulia pamoja
2. Kunja ngumi na kugongesha ngumi juu, chini, na juu tena
3. Nyoosha kwenye anga na kupeleka mabega na visigino chini mara tatu

## MSTARI WA KUMBUKUMBU 4

*1 Yohana 3:16 "Katika hili tumelifahamu pendo, kwa kuwa yeye aliutoa uhai wake kwa ajili yetu; imetupasa na sisi kuutoa uhai wetu kwa ajili ya hao ndugu."*

## SARAKASI 4: MASHINDANO YA UREMBO WA NGAMIA

Kamelia: Ooohhhh, nahisi wasiwasi!
Kamelot: Mbona unahisi wasiwasi, Kamelia? Najua utafanya vyema.
Kamelia: Hakuna jinsi nitakavyoshinda mashindano haya ya urembo! Mashindano ya kucheza densi yalikuwa kitu kimoja, ila haya ni tofauti. Oh, iwapo tu sikuwa na pua kubwa hivi na miguu mikubwa hivi! Wasichana wote nyumbani walinicheka kwa kuwa na pua na miguu mikubwa kuwaliko watu wengine, hata wavulana! Nitafanya nini, nitafanya nini?
Kamelot: Kuwacha alama kubwa katika ulimwengu?  Kushinda mashindano ya teke-ndondi?
Kamelia: Wewe! Nataka sana kushinda kwa sababu mmiliki wangu anapanga kutoa vyote tutakavyoshinda kwa hisani. Hili ni muhimu!
Kamelot: Kwani haujui vile ulivyo ndani ni muhimu kuliko ulivyo nje?
Kamelia: Kweli? Na pua langu, je?
Kamelot: Usifikirie kuhusu pua lako. Uko hapa kuwa ngamia mzuri zaidi na kuwa mtu mzuri kwa wengine ili wajue kuhusu Mungu! Makinika katika kuwa mzuri na mzingativu.
Kamelia: Na jinsi ninavyokaa, je?
Kamelot: Hapa, wacha nijaribu kuweka vipodozi katika uso wako. (Tupa poda kiasi katika hewa, inayotosha kuonekana na watoto. Kamelot na Kamelia wote watakohoa.) Labda sio hivyo. Ungetaka sindano za Botoksi?
Kamelia: La, hilo ni kudanganya na litafanya nitolewe!
Kamelot: Hapa, naweza kuweka rangi kwenye kope za macho yako…. (Kamelot anamkaribia Kamelia kwa namna inayotatanisha huku akiwa na rangi ya kope kwenye kinywa chake…) Usisonge.
Kamelia: Aka! La, hilo sio lazima. Ila, asanti kwa kunitia moyo. Nafikiri nitaenda katika mashindano ya urembo jinsi ambavyo Mungu alivyoniumba, na nitamakinika katika kuwa mzuri na mzingativu kwa watu wengine kama ulivyosema. Oh, ni wakati wangu sasa.
Kamelia anatoka kwenye jukwaa
Kamelot: Niambie mahali kilichoko chakula, kwa sababu naweza kukinusa kutoka mbali! Heehee! Nahisi Njaa.
Mtangazaji: Na mshindi kwa alama 19.7 ni…. Kamelia! Ametambulika kwa pua na miguu yake mikubwa, ambayo ni maumbile muhimu katika mashindano ya urembo wa ngamia.

## SOMO KUU LA 4

Karibu tena! Leo tutasoma sana zaidi kuhusu ujasiri. Milki ya Babeli ilitekwa na Wamedi na Waajemi. Wakati mfupi baadaye, mfalme Shashta aliunda karamu kubwa ili kuonyesha ufalme wake. Katika karamu hii kubwa, Malkia Vashti alikosa kutii. Mfalme alimtupa na kutafuta mwanamke mwingine aliyechukua nafasi yake. Mwanamke mchanga Myahudi aliyeitwa Esta na alikuwa mrembo na alikuwa na roho tulivu na upole ambao ulikuwa ni mzuri kwa watu wote waliokuwa karibu naye, na mfalme alimfanya kuwa malkia. Kumbuka marafiki wetu katika masomo yaliyopita? Walipewa mamlaka makubwa kwa ajili ya utukufu wa Mungu na manufaa ya wengine. Simulizi hii sio tofauti; Urembo wa Esta na mamlaka yake kama Malkia ulikuwa kwa manufaa kwa watu wengine. Kila mtu aseme, “Ujasiri unawaweka wengine mbele!”

Mtu aliyekuwa muovu aliyeitwa Hamani, alikuwa na mpango wa kuwaua Wayahudi. Alimshawishi mfalme kutoa amri kwa milki yote kuhusu siku moja ambapo kila mtu angewaua Wayahudi. Kila mtu aliingiwa na wasiwasi! Mjombake Esta , Modekai, ambaye ndiye aliyemlea, alimwambia Esta kuhusu jambo hili na kumwomba aingilie kati. Lilikuwa jambo la kuogofya, kwa sababu yeyote aliyekwenda kwa mfalme bila kuambiwa kufanya hivyo, aliuawa! Modekai alimkumbusha kuwa labda alikuwa amekuwa malkia ili awaokoe watu wake. Unaweza kuwa jasiri kwa kuwaambia watu kuhusu Yesu, ili wapate kuishi milele mbinguni, kumtetea mtu anayeteswa, kutiana moyo wa kumfuata Yesu badala ya kukosa kutii, kusema ukweli unaoumiza, au kufanya kitu kizuri kwa mtu aliye na upweke hata watu wanaposema vibaya kukuhusu. Kila mtu aseme, “Ujasiri unawaweka wengine mbele!”

Esta alimwuliza Modekai na Wayahudi katika milki kumwombea. Ukiona kitu ambacho unataka kukifanya kinatisha, mwombe Mungu kukupa ujasiri na usaidizi! Halafu Esta alifanya jambo la ujasiri na kusimama mbele ya mfalme. Kwa faraja yake, Mfalme alinyoosha fimbo yake ya ufalme na kusema asiuliwe na kumwuliza alichokitaka. Alimwalika katika karamu, halafu akamwalika katika karamu nyingine ya pili. Labda, katika wakati huo, alihisi woga wa kumwambia kuhusu Hamani, au labda tayari alikuwa amepanga. Hatujui. Ila ujasiri sio lazima uwe mkamilifu. Je, itakuwaje kama unahisi woga sana hadi utapike? Ni SAWA! Nenda bafuni na utapike, kisha rudi na hata hivyo, uwafanyie wengine mazuri. Jinsi unavyohisi woga mwingi, ndio unavyohisi ujasiri ukifanya kitu kizuri. Kila mtu aseme,” Ujasiri unamweka Mungu mbele ya ubinafsi!”

Mfalme alimsikiza Esta na kumnyonga Hamani katika kifaa cha kunyongea wahalifu ambacho Hamani alikuwa amekiunda kwa ajili ya Modekai. Mfalme pia aliwapa Wayahudi ruhusa ya kujilinda. Baada ya uovu wa Hamani akilini mwake, Wayahudi walipata manufaa katika milki yote. Halafu mfalme alimfanya Modekai kuwa na cheo cha pili chini yake katika milki yote, ambapo alitenda kwa manufaa ya Wayahudi. Labda hivyo sivyo mambo yatafanyika utakapofanya jambo la ujasiri. Huenda haitatokea jinsi ulivyotaka. Ila ujasiri wako unapowaweka wengine mbele, na kusimama kwa ajili ya Mungu kwa upendo, Mfalme anayefaa wa ulimwengu mzima, Yesu Kristo, atainuliwa katika maisha yako. Kila mtu atamwona akitenda katika maisha yako, na siku moja wote watamwabudu Mungu kwa matendo yako mazuri, na utapokea sifa kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Kila mtu aseme, “Ujasiri unawaweka wengine Mbele!”

## VIFAA KATIKA MILKI 4

*Fremu ya Picha*





***Nyenzo***

*Kiolelezo cha fremu kutoka kwa karatasi iliyo na upovu au rangi
*Taji 3 za karatasi
*Herufi "Mimi ni jasiri"
*½ mrija wa kunywea
*Utepe uliojikunjakunja
*Gundi

***Maelekezo***


* Kata kiolezo cha fremu na kuondoa vipande vya ziada.
*Ikunje nusu na kutia gundi na kushikanisha kingo 3 kati ya 4. Wacha kingo ya 4 ikiwa imefunguka na kutia picha na kuacha kanda zilizo juu kama zimefunguka ili kutia mrija wa kunywea.
*Unaweza kuchapisha picha au kuwaambia watoto wachore picha ya Esta na kuitia katika fremu.
*Rembesha taji na barua "Mimi ni jasiri."
*Kumalizia, tia mrija wa kunywea katika kanda zilizoko juu na kufunga utepe uliojikunjakunja katika pande zote mbili za mrija na kuning'iniza fremu ya picha.

## DARASA KATIKA KASRI 4











| | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| V | M | K | L | A | B | M | O | J | M | K | U | K | H |
| A | A | A | I | O | W | O | K | O | E | U | J | I | I |
| S | L | R | N | K | L | D | U | H | D | N | A | F | S |
| H | K | A | D | O | U | E | A | M | I | Y | S | A | I |
| T | I | M | A | A | W | K | S | A | A | O | I | A | W |
| I | A | U | E | S | T | A | I | L | N | N | R | C | O |
| H | A | M | A | N | I | I | H | U | I | G | I | H | G |
| W | A | A | J | E | M | I | M | S | K | A | W | A | A |
| A | T | S | A | H | S | E | M | L | A | F | M | K | H |
| W | A | Y | A | H | U | D | I | E | L | E | Z | A | U |

73





## MASWALI NA MAJIBU 4

1. **Je, ni yepi majina ya watu walio katika simulizi ya leo ya Biblia?**
   Mfalme Shasta, Malkia Vashti, Esta, Hamani, Modekai
2. **Nini kinachokutia hofu?**
   Majibu yanayowezakana: giza, buibui, nyoka, mbwa, silaha, wageni, sauti kubwa, kuisha kwa umaarufu, wanyanyasaji, kubadilisha makaazi na shule.
3. **Je, ni kitu gani cha ujasiri alichofanya Esta?**
   Aliomba nafasi ya kuwa malkia, aliyaweka maisha yake katika hatari kwa kwenda kumwona mfalme bila kualikwa, alimwalika katika karamu, alimwambia kuhusu mpango wa Hamani wa kuwaua Wayahudi.
4. **Je, ni jambo gani la ujasiri unaloweza kufanya?**
   Kuwambia wengine kuhusu imani yako kwa Mungu, kujitetea kutokana na wanyanyasaji shuleni, kuwaambia wazazi wako ukweli.
5. **Je, mbona Mfalme Shasta hakubadilisha amri yake ambayo Hamani alimwambia kutoa: katika siku fulani ya kuwaua Wayahudi wote katika nchi yote?**
   Milki ya Wababeli ilitekwa na Wamedi na Waajemi na sheria zao hazingebadilishwa.

## KAZI YA ZIADA 4

Fanya mazoezi ya ujasiri na kumwambia mtu fulani kwamba wewe ni Mkristo.

## SARAKASI NA DANIELI 4

Mwalimu:  Leo, kuna mtu mwingine ambaye atakuja kututembelea. Kila mtu, tafadhali mkaribishe Malkia Esta.

Esta: Hamjambo kila mtu. Nafurahia kuwa nanyi leo.

Mwalimu: Tunasoma leo kuhusu simulizi yako. Je, unaweza kutwambia jinsi ulikuja kuwa Malkia?

Esta: Nilikuwa naishi na mjombangu Modekai aliyenilea wakati Mfalme Shasta alimtoa malkia Vashti kwa kutomtii mbele ya wakuu. Wasichana wote waliitwa katika karamu ya urembo ili kuona ni nani ambaye angekuwa malkia. Nilihisi woga kumwacha Modekai, ila alinitia moyo. Tulitumia mwaka mzima katika matayarisho na vipodozi vya urembo. Wasichana wengine walikuwa wabaya, wengine wazuri, na wengi nilidhani wazuri kuniliko. Ila nilipata mapendeleo kutoka kwa mtu

aliyekuwa msimamizi wetu na kufuata mapendekezo yake wakati wa kukutana na mfalme. Sijui ni kwa nini alinichagua mimi, ila mara moja tu nikakuwa malkia wa Milki.

Mwalimu: Lo, ilikuwa kutimia kwa ndoto nzuri kweli! Je, maisha yanakaa aje kama malkia?

Esta: Mara kwa mara namtumikia mfalme na kwenda katika karamu na matukio na kuwaalika mabibi za maafisa wanaotembelea milki yetu kutoka mbali.

Mwalimu: Je, nini kilimtendekea Hamani?

Esta: Alimshawishi mfalme kutoa amri iliyompatia kila mtu ruhusa ya kuua Wayahudi kwa namna fulani. Nilihisi woga kuwa watu wangu wangeuliwa, ila hakuna mtu katika milki aliyejua kuhusu jambo hili, kwa sababu sikuwa nimewaambia kuwa mimi ni Myahudi. Halafu hali ikawa mbaya hata zaidi. Hamani alipanga kumwua mjomba wangu Modekai kwa kumnyonga katika kifaa cha kunyongea wahalifu katika nyumba yake. Ila usiku alikwenda kumwomba mfalme ruhusa, nae mfalme alikuwa akisikiza rekodi na kukumbuka jinsi mjomba wangu alivyoyaokoa maisha yake wakati uliopita. Badala ya Hamani kumwua Modekai, mfalme alimwelekeza Hamani kumtembeza Modekai ndani ya milki yote kwa farasi na nguo za kifalme huku akiwaeleza watu heshima aliyokuwa nayo mfalme kwa Modekai.

Mwalimu: Je, hilo liliwaokoa watu wako kutokana na amri hiyo?

Esta: La, kwa sababu amri katika milki za Umedi na Uajemi haziwezi kubadilishwa. Tulikuwa bado katika matata kutokana na amri hio ya kuogofya.

Mwalimu: Je, ulifanya nini?

Esta: Modekai alinitia moyo tena na kuniomba kwenda kumwomba Mungu usaidizi. Lilikuwa ni jambo la kuogofya. Hata kama mimi ni malkia, sijakubalishwa kumtembelea mfalme bila kualikwa, na adhabu ilkuwa ni kifo. Ila Modekai alisema kuwa Mungu alikuwa amenifanya kuwa Malkia kwa sababu tu ya jambo hili na kuniomba kuwa jasiri. Niliwaomba Wayahudi wote kuniombea na kujifunga kwa siku kadhaa. Halafu, nikavaa na kwenda kwa mfalme. Nilijaribu kuficha nilivyokuwa natetemeka. Mfalme alitabasamu na kunyoosha fimbo yake ya ufalme ili kuniokoa, na ilikuwa ngumu kwangu kuendelea kusimama. Halafu nikamwalika mfalme na Hamani katika karamu, halafu karamu nyingine. Mwishowe, baada ya maombi mengine ya haraka, nilimwambia mfalme kuhusu amri hii na kuwahusu watu wangu. Hamani alikuwa mtu aliyemfuata katika cheo, na niliogopa sana mfalme angemchagua Hamani badala yangu na watu wetu. Ila mfalme alikasirika na kuagiza Hamani kuuliwa katika kifaa alichotaka kumyongea Modekai. Halafu mfalme akampandisha cheo Modekai ili kuchukua nafasi yake, na tukaandika amri ya pili kwa niaba ya mfalme ili kuwajulisha watu wetu kujitetea badala ya kuuawa.


Mwalimu:  Asanti sana kwa kuja, Esta.

Esta: Asanti sana kwa kunialika.

## SHUGHULI 4


***Kuwaweka wengine mbele***

Kuwasaidia watu kufikiria jinsi ya kuwaweka wengine mbele, unda mpira wa karatasi na kuambia kikundi kuutupa juu hadi kwa kila mtu anayefuata. Wakati mtu ako na mpira, atataja namna ya kuwaweka watu wengine mbele. Kwa mfano, naweza kumweka mwanafunzi mwenzangu mbele kwa kumkubalisha kuingia msalani mbele yangu.



# KARAMU YA KIFALME 4

***Roho nzuri ya Malkia***





***Viungo:***

- Kisu cha kukata biskuti kilicho na umbo la roho au karatasi ngumu inayoweza kukata, na kisu
- Tunda lililokatwa
- Vijiti (mishikaki)

***Maelekezo:***

1. Kata maumbo ya roho kutoka kwa tunda kwa kisu cha kukata biskuti. Iwapo hauna kisu cha kukata biskuti kilicho na umbo la roho, unda roho kutoka kwa kadibodi au karatasi gumu.
2. Tia maumbo haya ya matunda katika mishikaki.

***Sasa furahieni matunda haya yaliyo na maumbo ya roho ili kukumbuka roho nzuri ya malkia!***

# MICHEZO YA BUSTANI 4

## *Bingo Lingo*



Kwa usaidizi wa darasa, unda orodha ya maneno muhimu 50 au 60 katika somo, katika simulizi la Esta. Iweke orodha katika eneo lililo rahisi kuiona. Andika kila neno katika karatasi ndogo, kisha kuikunja hadi nusu, na kuiweka katika mkebe au chombo kingine. Watoto watаunda kadi zao za Bingo, huku wakikunja ukurasa nusu mara mbili katika kila upande ili kutia alama ya mistatili 16 katika karatasi yao. Katika kila mstatili, wataandika neno. Maharagwe, mawe, n.k. yanaweza kutumiwa kama vifaa vya kutia alama. Wanaweza kutumia kadi mara kadhaa au kubadilisha na mwenza. Mwalimu atatoa neno kutoka kwa mkebe na kulisema kwa sauti kubwa. Iwapo mtoto ako na neno hilo katika kadi yake, analifunika kwa kalamu ya rangi. Mtu wa kwanza kujaza kadi yake anasema kwa sauti ”Bingo Lingo.” Na ndiye mshindi.

## *Mashindano ya mbio za ngamia*



Unda timu zinazotoshana za watoto 10-15 katika kila timu. Halafu wapange mstari ulio na nafasi ya kutosha ya kucheza. Tia alama ya goli katika upande mwingine wa chumba. Ili kucheza, mchezaji wa kwanza katika mstari atakimbia na kutoa sauti kama ngamia hadi kwa goli, kugeuka na kurudi katika timu. Anapomgusa mkono mchezaji aliye kando, mchezaji huyo mwingine anachukua nafasi ya kukimbia katika mbio hii. Timu ya kwanza ambapo watoto wote watamaliza mbio kwanza, watakuwa ndio washindi. Cheza tena kwa kubadilisha aina ya mbio: ruka kwa mguu mmoja, geuka hadi mistari wa mwisho wa kushinda, n.k.

# 5. UJASIRI UNASTAHIMILI

Danieli 6: Maombi ya kila siku na pango la

## VIMAKINISHI /MAKOFI 5

"Ujasiri unastahimili"

1. Pamoja na rafiki yako, pigeni makofi kwa mikono yenu yote miwili
2. Kisha pitishaneni mikono na kupiga makofi pamoja tena
3. Rudia makofi ya kwanza
4. Piga makofi kwa mikono ya kulia, halafu kushoto, halafu kulia
5. Malizeni kwa kofi la mwisho kwa mikono yote miwili

## MSTARI WA KUMBUKUMBU 5

*Waebrania 10:36 "Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi."*

## SARAKASI 5: MSAFARA WA NGAMIA

Kamelia: Lo, jua hili la jangwa litaiharibu ngozi yangu nzuri!
Kamelot: Kitu kizuri uko na koti ulilovaa.
Kamelia: Najua, kuna joto jingi hata nikiwa na manyoya haya. Je, mbona hata tuko hapa nje? Nataka kurudi Uajemi. Je, nitabebwa na msafara huu kwa muda gani?
Kamelot: Siku mzima. Halafu tutajua tutakachokifanya kesho?
Kamelia: Kutembea?
Kamelot: Ni kweli!  Na siku itakayofuata, unajua nini?
Kamelia: Tutatembea?
Kamelot: Kweli! Unajua aje?
Kamelia: Aaaaah! Kila asubuhi tutaamka na kula kile kile na kuomba pamoja, kisha tutatembea na kutembea, halafu tutasimama na kula chakula cha mchana na kula kitu kile kile na kuomba tena, halafu kutembea na kutembea, halafu ikifika usiku tutakula kitu kile kile na kuomba na kisha kulala. Nimechoka sana kufanya kitu kile kile! Hata naanza kuomba nikitembea! Na unajua nini? Nahisi kiu? Hilo huwa halifanyiki! Naweza kusimama sasa?
Kamelot: Nini, wachia hapo? Wacha tuone… pale hakuna maji. Na angalia! Hata maji hakuna. Ngoja, kuna nini pale? Hakuna maji. Ni mahali pabaya kusimama.
Kamelia: Ugh… au tusiombe KILA tunaposimama? Halifurahishi. Halafu, msafara wetu mkubwa uliwacha kuomba na unafikiria tunafanya kisichofaa kuendelea kuomba. Kwani ni jambo kubwa?
Kamelot: Sio kwa burudani. Tunamhitaji Mungu kila wakati!
Kamelia: Kuliko maji?
Kamelot: Kweli! Hata kuliko mafuta ya kupunguza miale ya jua. Au vifaa vya simu.
Kamelia: Sasa, hivi karibuni nitakufa moyo na utanibeba hadi uko.
Kamelot: Wewe! Niko na kiu. Endelea kutembea, hatua moja hadi nyingine.
Mtangazaji: Baada ya wakati mfupi, walifika katika kisima.
Kamelia: Lo! Nilidhani nitakufa!
Kamelot: (Akitafuna) Sisi sote tutakufaaa!!! ( Anaingiza pua kiasi nyuma ya jukwaa)
Kamelia: Wewe, Uliskia ngamia hao wakiongea?
Kamelot: Wenye walikuwa na leseni kutoka kwa nchi geni?
Kamelia: Ndiyo. Walikuwa wakiongea kuhusu aina zote za nyoka na wezi na dhoruba ya mchanga…
Kamelot: Na kupiga chafya na vidole vilivyogonga mawe na (Lo!) hakuna wifi! (Anaendelea kula)

Kamelia: Nashindwa kama Mungu alitulinda wakati wote huu. Wewe, unajua nini? Nahisi vizuri katika kisima hiki na vyakula na maji… na ni rahisi sana kumwomba Mungu. Ni kama kustahimili na kutumia wakati na Mungu wakati kulikuwa kugumu sasa kumekufanya kuwa rahisi sasa.
Kamelot: Ndiyo. Pia mimi. Wewe, utawezaje kula hicho? Niko na njaa.

## SOMO KUU 5

Karibu tena katika VBS! Tumesoma aina nyingi ya mambo kuhusu ujasiri wiki hii. Leo tutasoma kuwa ujasiri unastahimili. Kila mtu aseme, "Ujasiri unastahimili!" Kustahimili kunamaanisha kuendelea kufanya vitu vizuri unavyofanya. Haijalishi ulichokifanya jana. Iwapo ulifanya vizuri katika kumfuata Yesu, usijali kwa sababu alikuokoa kutoka kwa dhambi zako. Ila usikubalishe uliyoyafanya jana yaliyokuwa mabaya kukuzuia kufanya mema leo! Kila mtu aseme, "Ujasiri unastahimili!"

Ujasiri haumweki tu Mungu mbele lakini ustahimili pia unamweka Mungu mbele kila siku. Usimtumaini Mungu mara moja tu, ila kila siku. Usiseme ukweli mara moja tu, bali kila wakati. Na usiwaweke wengine mbele yako mara moja tu bali kila siku. Yesu alitwambia tumkabidhi maisha yetu kila siku, tumnyenyekee na tufanye mambo mazuri hata kama hatuhisi kuyafanya. Danieli, ambaye tulisoma kumhusu siku ya 1, akimwomba Mungu mara tatu kila siku bila kukosa. Kwa wakati huo huo, alikuwa msimamizi mkubwa sana hadi Mfalme Dario alitaka kumfanya msimamizi wa ufalme wote. Hili lilifanya watu wengine kuhisi wivu sana hadi wakamshawishi Dario kutoa amri ya kumkamata Danieli kwa kufanya kukosa kuomba kuwa sheria. Kila mtu aseme, "Ujasiri unastahimili!"

Badala ya kuogopa amri ya mfalme, Danieli aliendelea kumwomba na kumshukuru Mungu mara tatu kwa siku kama kawaida. Unapomtambua Mungu kama mwenye nguvu yote na mwenye nguvu hata kuliko wafalme na sheria, unaweza kutambua kuwa kila kitu kizuri kinatoka kwa Mungu na kumshukuru Mungu hata katika hali ngumu. Siku moja, Danieli alikuwa akiomba na kumwomba Mungu usaidizi. Wakati huo huo, maadui zake walimshika na kumtia mbaroni. Alikuwa akimwomba Mungu usaidizi shida ilipomjia! Hata mfalme Dario alikasirika na alijaribu kila aliloweza ili kumuokoa Danieli ila, hakuna kitu kingefanywa. Mara nyingi katika maisha yetu, kwa sababu Mungu ako na busara kuu na ako na ujuzi na anaweza kutafuta njia hata mtu anaposhindwa kuipata. Kila mtu aseme, "Ujasiri unamweka Mungu mbele!"

Danieli alitupwa katika pango la simba na kukaa hapa usiku mzima. Jambo la kuogofya sana! Je, ushawahi kumwona simba akiwa karibu? Hata mngurumo mdogo unatikisa sakafu. Ila mungu alimwokoa Danieli ndani ya pango hili kwa kutuma malaika wake kufunga simba wale vinywa. Danieli alikaa na simba usiku wote kama jinsi ni wanyama bandia wakubwa. Kulipokucha, Mfalme Dario alikuja na kupata Danieli yuko salama. Aliwatupa maadui wa Danieli katika pango, na simba wale waliwaua hata kabla waguse chini. Wakati huo huo, mfalme Dario aliambia milki nzima kuabudu Mungu wa Danieli, na Danieli alipandishwa cheo hadi nafasi kubwa katika ufalme. Kila mtu aseme, "Ujasiri unastahimili!"

Kujua Mungu ni nani, kwamba yeye ndiye Mungu mkuu na mwenye nguvu yote, kunatupa ujasiri wa kufanya mambo magumu, kama vile kutumaini na kumfuata Mungu na kuwapenda wengine hata katika ugumu. Ili kuelewa zaidi na zaidi Mungu ni nani, tunafaa kutumia wakati naye kila siku, kama alivyofanya Danieli. Kusoma Biblia, kuomba, kumwimbia nyimbo hata tukiwa peke yetu. Ukiendelea kufanya hivyo, utaendelea kujua zaidi jinsi Mungu alivyo mkuu na wewe na jinsi unaweza kuwa jasiri zaidi kwake. Kila mtu aseme, "Ujasiri unastahimili!"

## VIFAA KATIKA MILKI 5

### *Barakoa ya Simba*



***Nyenzo***

*Shina la barakoa
*Karatasi ya povu ya manjano au karatasi ya rangi iliyo na uso
*Karatasi ya povu ya rangi ya machungwa au karatasi ya rangi ya maskio, nyusi, na pua
*Karatasi ya povu nyeupe au karatasi ya mdomo
*Utepe uliojikunjakunja, 50 sentimita
*Rangi
*Gundi

***Maelekezo***

* Kata shina la barakoa na kulipaka rangi.
* Weka gundi na kushikanisha povu/karatasi ya manjano hapo juu kama ilivyoonyeshwa katika picha iliyopo hapa.
*Juu ya hilo, weka gundi katika kinywa na kisha katika pua hapo juu. Pia weka gundi katika masikio na kovu kama ilivyoonyeshwa katika picha.
*Funga utepe uliojikunjakunja katika mashimo katika pembe zote mbili ili itoshee katika kichwa cha mtoto.

## DARASA KATIKA MILKI 5











| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | H | D | A | N | I | E | L | I | U |
| K | A | Y | M | S | P | M | I | K | S |
| I | R | L | F | I | Y | K | N | U | T |
| L | A | M | A | M | R | I | A | W | A |
| A | M | A | L | B | V | L | Y | A | H |
| S | U | L | M | A | I | A | O | N | I |
| I | B | A | E | O | N | M | O | A | M |
| K | I | I | D | M | Y | A | G | I | I |
| U | B | K | A | B | W | R | O | M | L |
| S | L | A | R | A | A | A | F | A | I |
| F | I | D | I | M | B | A | Y | N | U |
| U | A | S | O | M | A | P | A | I | M |
| K | U | T | I | I | O | G | N | A | P |
| E | N | Y | E | W | I | V | U | F | S |



| | | |
|---|---|---|
| 4 | 2 | 14 |
| 9 | 15 | 3 |
| 1 | 11 | 8 |
| 10 | 5 | 7 |
| 12 | 13 | 6 |



## MASWALI NA MAJIBU 5

1. **Je, inamaanisha nini "kustahimili"?**
   Inamaanisha kutokufa moyo ila kukaa ukifanya jambo hata ikiwa ni vigumu. Danieli hakukufa moyo kuomba.
2. **Je, wakati simba walikuwa na njaa sana, mbona hawakumla Danieli?**
   Mungu alimtuma malaika wake kuwafunga vinywa ili wasikule chochote.
3. **Je, Mfalme Dario anaweza kuwa alikuwa anahisi nini wakati huu: Wakati alishawishiwa kufanya iwe kinyume cha shera kumwomba Mungu? Alipokuwa akimtupa Danieli katika pango la Simba? Alipopata Danieli yuko salama? Alipoamua kuwaweka maafisa wote katika pango?**
   Majibu yanayowezekana: Majivuno na kuhisi wa kipekee kuombwa, hofu kumweka Danieli mahali ambapo angekufa, kufurahia kwamba Danieli alikuwa salama, kuwakasirikia maafisaa kwa kumshawishi kumwumiza Danieli.
4. **Je, ni jambo gani unalipata kuwa gumu kuendelea kufanya katika maisha?**
   Majibu yanayowezekana: Maombi, kumwimbia Mungu, kumwoshea mama vyombo, kumtendea kwa uzuri ndugu yako, kutowatusi wengine katika mabishano, kulinda roho na mawazo yako, kutofanya shughuli ambazo "kila mtu" anazifanya ambazo unajua ni makosa.
5. **Je, nini ilifanyika baada ya Mfalme kumtoa Danieli katika Pango?**
   Mfalme aliwaambia watu wote kumuabudu Mungu wa Danieli. Danieli alipandishwa cheo hadi nafasi ya juu katika ufalme.

## KAZI YA ZIADA

Kama alivyofanya Danieli, omba mara 3 kwa siku.

## SARAKASI NA DANIELI 5

Mwalimu: Karibu tena, Danieli.

Danieli: Asanti. Niko na furaha kuwa hapa tena leo. Je, ilikuwaje Malkia Esta alipowatembelea?

Mwalimu: Tulijawa na furaha alipotutembelea. Leo, tuliskia jambo kukuhusu na simba? Je, ni ukweli?

Danieli: Ni ukweli. Nilikaa na simba wakati mmoja. Hivi sasa, nimewaambia hadithi zilizofanyika tu wakati Mfalme Nebukadneza alikuwa katika mamlakani. Baadaye, Wamedi na Waajemi walikuja na kuteka Babeli. Mara nyingine,

ilikuwa ni mbadilishano wa mamlaka na ilikaa ni kama kurudi kuwa mateka, kusoma utamaduni na mfumo wa uongozi mpya tena. Ila Mfalme Dario alinitambua na kuniweka mimi pamoja na wengine wawili kusimamia mikoa yote tofauti. Baada ya muda, alipanga kunifanya msimamizi wa milki yote. Maafisa wengine walihisi wivu na walitaka kuniua. Niliskia wakinong'onezana nikipita na nilijua kuna jambo walikuwa wakipanga. Siku moja, Mfalme Dario, alitoa amri kwamba hakuna mtu alifaa kuabudu mungu au mtu yeyote na badala yake Dario pekee kwa mwezi mmoja na adhabu ya kutupwa katika pango la simba kwa ambaye hangetii. Watu wanakaa wakiabudu au kuomba vitu vidogo. Wakati huu, ilikuwa mtu aliyeishi. Nilihisi ni jambo lisilofaa, ila katika milki hii mpya, hakuna ambaye angebadilisha amri. Kama jambo katika ratiba yangu ya kila siku, mimi hupitisha wakati nikimwomba na kumshukuru Mungu kila siku. Amekuwa akinisaidia katika maisha yangu yote, na naendelea kuhitaji usaidizi wake ili kufanya kazi yangu vizuri.. Nilikuwa nikiabudu na kumwomba Mungu usaidizi siku moja wakati maafisaa waliponifumania katika chumba changu na kunishika nikimwomba Mungu. Walinipeleka kwa mfalme Dario. Alionekana kuvunjika moyo walipomwambia nini nilichokuwa nimefanya. Nilitamani sana kutoka katika hali ile, kuendelea kumtumikia mfalme huyu mpya na kufanya kazi kwa manufaa ya watu katika milki yote.

Mfalme Dario alitumia siku mzima kutafuta namna ya kuniokoa. Sikujua kwamba alinipendelea sana hivi. Ila, usiku, wakati hakukuwa na namna ingine, alinitupa katika pango. Sitawahi kusahau mahali hapo, mnuko, joto, na sanasana simba wakubwa. Hata mngurumo mdogo katika koo zao huwa unatikisa sakafu. Ila hawakuja karibu nami kunishambulia au kunikula au kula kitu chochote usiku. Ni lazima kulikuwa na malaika au kitu kama hicho, kama marafiki zangu walivyohisi katika tanuri. Kulipokucha niliskia sauti ya Mfalme Dario, ikiitana na kuniuliza kama nilikuwa salama na kama Mungu wangu alikuwa ameniokoa. Nilimwambia kuhusu malaika na kwamba sikuwa nimefanya jambo lolote la kumkosea. Aliagiza watu hao wengine watupwe katika pango, na simba waliwakula mara moja. Halafu akaandika amri kuwa kila mtu katika ufalme anafaa kumwogopa na kumuabudu Mungu wetu. Ona, kwa namna hii, Mungu alifanya nguvu zake zikajulikana kwa mfalme mpya ambaye mbeleni hakumjua. Mara nyingine, tuliona kuwa Mungu alikuwa nasi hata mahali tulikokuwa baada ya kutekwa.


Mwalimu: Ni jambo la kutia moyo kusikia jinsi ulivyostahimili katika maombi.

Danieli: Ni rahisi kusahau, ila ukweli ni namhitaji Mungu kila siku. Ananisaidia kila wakati na kwa hivyo ninamshukuru kila wakati.

## SHUGHULI 5

***Kupanga wakati wangu***

Mpe kila mtoto karatasi. Waambie watoto kufikiria wakati ambao hawana shughuli ambao wanaweza kuutumia na Mungu, kwa kuomba, kusoma Biblia au kumwabudu Mungu. Waambie waandike au wachore katika karatasi wakati ambao hawana shughuli na kuwahimiza kutumia wakati huu na Mungu. Kuanzia inaweza kuwa ni dakika 2 pekee na Mungu, halafu wakati mwingi zaidi.



## KARAMU YA KIFALME 5

***Simba***



***Viungo:***

- Tunda la manjano utakalolichagua (Nanasi, embe, n.k.)
- Chungwa au Mboga (Chenza au Vipande vya karoti)
- Kipande cha Ndizi (kwa maskio)
- Kisu
- Buluuberi au zabibu kavu

***Maelekezo:***

1. Kwa kutumia kisu kata umbo la duara katika tunda la manjano kwa uso la uso wa simba.
2. Weka tunda la manjano na/au mboga ambayo umeichagua, kuifananisha na shungi la simba.
3. Weka vipande vya ndizi kufanana na masikio.
4. Weka bluuberi au zabibu kavu kama sehemu ya macho ya simba.
5. Kwa masharubu ya simba, weka vipande vya karoti.

***Tayari! Sasa tunaweza kula simba anayeonja vizuri tukikumbuka kuwa ni lazima tuwe majasiri sana kama Danieli.***

## MICHEZO YA BUSTANI 5

### *Nyuso na ishara*



Katika karatasi ndogo, andika majina ya watu na vifaa katika hadithi za Biblia katika VBS, kama vile Danieli, Esta, Mfalme Nebukadneza, moto, simba, n.k. Weka vipande hivi vya karatasi katika mkebe. Unda timu 2 na watoto. Mwakilishaji kutoka kila timu anakuja katika eneo ili kufanya uigizaji. Toa kipande cha karatasi ili kutafuta watakachofanya. Bila kusema neno lolote au kutoa sauti, watoto hawa wawili wataiga kama kifaa au mtu huyu, na watoto wengine watakisia ni nini au ni nani. Rudia mchezo, huku mkibadilishana wanaoiga. Timu inayokisia sana itashinda.

### *Mnara wa Kikombe*



Unda timu mbili na watoto na kumwambia mwakilishi kutoka kwa kila timu kucheza pale mbele. Mpe kila mchezaji nambari inayotoshana ya vikombe vya plastiki na kisha kuwafunga macho. Wachezaji ni lazima wajenge mnara wakiwa wamefungwa macho. Iwapo mnara wake utaanguka, mchezaji atapoteza. Mchezaji anayemaliza wa kwanza bila mnara wake kuanguka anashinda.